

**MAN UNITED WASAKA MBADALA WA ONANA**

UKURASA 22

**BASHE** awataka viongozi kampuni ununuzi tumbaku wajisalimishe

UKURASA 5

**MAKALA** Vigogo walioingilia zabuni ya bil. 9.8/- wachukuliwe hatua

UKURASA 7

**BARAZA** lashtuka kasi ya wanawake wanaodai talaka

UKURASA 10

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumatatu Desemba 30, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581907

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

epaper.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

### AJALI ILIYOUA WALIMU...

# Polisi wamshangaa dereva bodaboda

UKURASA 3



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, SACP Augustino Senga akionesha baadhi ya vipodozi vilivyopigwa marufuku kuingizwa nchini, vilivyokamatwa na jeshi hilo mtaa wa Keseria, kata ya Chapwa, wilayani Momba juzi. Habari Uk. 4. **PICHA: JESHI LA POLISI**

UKURASA WA 12

## WANAMICHEZO BORA WA KUANGALIWA MWAKA 2025

KALENDA ya michezo inapozidi kupamba moto kuelekea mwaka 2025, ulimwengu unatazamiwa kuona msururu wa matukio ya kusisimua na...



# Lema atoa tahadhari CHADEMA kuporomoka

UKURASA 2

## Mtendaji wa Kijiji adaiwa kujinyonga kisa mazingira ya kazi

UKURASA 16

**MICHEZO** **FADLU AWAAHIDI SIMBA MAKUBWA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Mafundi wakiendelea na kazi ya kuboresha miundombinu ya kupitisha maji ya mvua pembeni mwa Barabara ya Morogoro eneo la Kimara Korogwe Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya upanuzi wa barabara hiyo unaoendelea. **PICHA: SABATO KASIKA**

UCHAGUZI WA MWENYEKITI...

# Lema atoa hadhari CHADEMA kufa

**Na Elizabeth Zaya**

WAKATI Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kikiwa katika maandalizi ya uchaguzi wa viongozi wake ngazi ya taifa, Mwenyekiti mstaafu wa chama hicho Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema amewaonya wanachama na wafuasi wa chama hicho dhidi ya minyukano inayoendelea.

Amesema wanachopaswa kufanya hivi sasa ni kurudi kwenye malengo yao, huku akisisitiza kuwa wakipoteza mwelekeo wa kusudi lao, kuna hatari na chama chao kufa.

Alitoa tahadhari hiyo juzi kupitia ukurasa wake wa X (zamani twiter), akisema vita inayoendelea hivi sasa ndani ya wanachama wenyewe kwa wenyewe ni kubwa na ni hatari kwa mustakabali wa chama.

Lema ambaye ni Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini, alisema kwa hali ilivyo, wanachama wa chama hicho wao kwa wao wanapigana vita vikali kutokana na mgawanyo uliotokana na viongozi wanaowaunga mkono ambao wanagombea nafasi za juu za uongozi kitaifa katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

"Kwa hali ilivyo sasa, tuna uchungu sisi kwa sisi kuliko tulivyo na uchungu dhidi ya CCM (Chama Cha Mapinduzi).

"Kampeni ya sasa ya dhihaka na matusi kwa viongozi na wananchi ambao hatuwaungi mkono imekuwa kali kuliko kampeni ya kukomesha mauaji na utekaji nchini," "Let's get back to the purpose (turudi katika kusudio) na kila mtu aheshimiwe na kuthaminiwa kwa upande aliochagua kwa maana ndiyo demokrasia," Lema alisema.

Pia aliwatahadharisha wanachama na wafuasi wa chama hicho kwamba ni vyema wakatambua kwamba mnyukano wa wao kwa wao unaoendelea mitandaoni, unafuatiliwa na wapinzani wao na watautumia katika kampeni za uchaguzi mkuu mwakani.

Alisema hatari nyingine kubwa kwa chama hicho ni kwamba hata wananchi wanawafuatilia kwa karibu na kusambaza kila habari inayoleta fitina ndani ya chama hicho.

"CCM wanatufuatilia sana, wanahifadhi kila kauli zetu juu ya wagombea wetu wote katika mchakato wa uchaguzi wa viongozi wakuu Januari. Bila shaka watazitumia kauli hizi mwaka 2025 kama tutashiriki na kama kutakuwapo na uchaguzi huru," Lema alionya.

Kada huyo wa CHADEMA alisema wananchi wanatumiana kila habari inayoleta fitina na uchungu miongoni mwao, akihadharisha kuwa "hii ni hatari!".

Alisema chama cha siasa za upinzani ni harakati za kutafuta utawala bora zinazoongozwa na kile alichokiita "kusudio la ndani na moyo wa kujitoa".

"Kusudi likifa, chama kinakufa kwa sababu asilimia 99 ya viongozi na wanachama wanafanya wajibu wa kazi za chama kwa kujitolea. Sasa watawezaje kujitolea kama hakuna purpose (kusudi)? Ari inajengwa na nidhamu," alifafanua.

Tangu kutangazwa kuanza kwa mchakato wa kuchukua fomu za kuwania nafasi za uongozi ndani ya CHADEMA, mpaka sasa waliochukua fomu ya kuwania nafasi ya uenyekiti ni Freeman Mbowe, Tundu Lissu, Romanus Mapunda na Charles Odero.

Mnyukano umekikumba chama hicho baada ya viongozi wakuu wa chama hicho, Mwenyekiti Mbowe na Makamu wake Lissu kutangaza kuchuana katika nafasi ya juu kabisa ya chama chao.

Baadhi ya wanachama wanamuunga mkono Mbowe, wakitaka aendelee kwenye nafasi hiyo kwa awamu nyingine. Kuna kundi lingine linamuunga mkono Lissu, likiamini ni wakati wa kupata kiongozi mpya wa kuongoza chama hicho.



Mwenyekiti mstaafu CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Radi yaua watano wa familia moja

**Na Grace Mwakalinga**

WATU watano wa familia moja katika kitongoji cha Nkangi, wilayani Chunya, mkoani Mbeya wamefariki dunia baada ya kupigwa na radi kwenye kambi ya kuchunga ng'ombe wakiwa wamelala, huku wengine watano wakijeruhiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi (SACP) Benjamin Kuzaga, alithibitisha kutokea kwa vifo hivyo, akisema tukio hilo lilitokea saa 8:30 usiku wa kuamkia jana.

Kamanda Kuzaga alisema tukio hilo lilitokea katika kitongoji cha Nkangi, watu hao watano wa familia moja ya mfugaji Masiganya Scania (39) walifariki dunia.

Aliwataja waliofariki dunia katika tukio hilo ni Balaa Scania (28), Kulwa Luweja (17), Masele Masaganya (16), Hema Tati (10) na Manangu Ngwisu (18), wote wakazi wa kijiji cha Nkangi.

"Katika tukio hilo, watu wengine watano walijeruhiwa ambao ni Gulu Scania (30), Manyenge Masaganya (13), Seni Solo (13), Paskali Kalezi (16) na Huzuni Kalezi (19)," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia jana iliyoambatana na radi na kusababisha vifo vya watu hao na kujeruhi kadhaa.

Kamanda Kuzaga alisema majeruhi walikimbizwa katika Kituo cha Afya Isangawana kwa ajili ya matibabu na baadaye waliruhusiwa kurejea nyumbani baada ya hali zao kuimarika.

Katika tukio lingine, Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya linamshikilia Anna Mwakilima (24), mkazi wa Mbuyuni, wilaya ya Mbarali kwa tuhuma za wizi wa mtoto mwenye umri wa miezi miwili na nusu (jina la mtoto tunalihifadhi kwa sababu za kisheria).

Kamanda Kuzaga alisema kuwa Desemba 22 mwaka huu, Aneth Mgaya (20), mkazi wa kijiji cha Mwakaganga, wilayani Mbarali, aliibiwa mtoto wake mwenye umri wa miezi miwili na nusu na mwanamke ambaye alimfahamu kwa sura.

Alisema siku moja kabla ya tukio, majira ya saa 10 jioni, mtuhumiwa alifika nyumbani kwa Aneth na kuomba hifadhi ya kulala kwa madai kuwa alitokea mjini Mbeya na alikuwa anaishi kwa muda Ubaruku, Mbarali kwa ajili ya biashara ya vitenge.

Alieleza kuwa siku iliyofuata Desemba 22, 2024, saa moja asubuhi, Aneth aliamka na kutoka nyumbani kwake kwenda kununua vitafunwa eneo la jirani, huku akimwacha mtuhumiwa na watoto wawili. Baada ya kurejea nyumbani, hakumkuta mtuhumiwa wala watoto wake.

Kamanda Kuzaga alisema Aneth alitoa taarifa katika kituo cha polisi na ufuatiliaji ulifanyika na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo.

Alisema kuwa juzi saa 12 jioni, katika kijiji cha Mbuyuni, kata ya Mapogoro, wilayani Mbarali, polisi walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa Anna Mwakilima akiwa na mtoto huyo ambaye hajamdhuru.

# Ulega akagua ujenzi barabara za mwendokasi usiku, atoa maagizo

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega amefanya ziara ya kushtukiza ya ukaguzi wa maendeleo ya miradi ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) jijini Dar es Salaam na kutoa maagizo.

Katika ziara hiyo, Waziri Ulega ameagiza miradi hiyo ikamilike kabla ya msimu wa mvua za masika mwakani ili kupunguza changamoto za msongamano wa magari katika jiji hilo la kibiashara.

Ulega alisema: "Nimeagiza kazi ifanyike usiku na mchana kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati. Msimu wa masika una changamoto zake, hatutaki kuona wananchi wakitaabika.

"Tunafanya hivi kwa kutekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Ilani ya CCM ya Mwaka 2020-2025 inayosisitiza kupunguza msongamano wa magari mijini."

Waziri Ulega alikagua maendeleo ya upanuzi wa Barabara ya BRT 1 kutoka Ubungo hadi Kimara pamoja na Barabara ya Mwenge-Tegeta inayojumuishwa katika mradi wa BRT 4.

Akiwa katika ukaguzi huo, Ulega alisema ameridhishwa na kasi ya kazi zinazofanywa na makandarasi ambao wameanza kutekeleza agizo lake la kufanya kazi kwa saa 24 kila siku.

"Timu ya usimamizi ya TANROADS chini ya Mtendaji Mkuu wake, Mohamed Besta, inafanya kazi nzuri. Makandarasi lazima wafanye kazi muda wote bila kupoteza muda. Watanzania wanatamani kuona miradi hii ikikamilika na sisi kama serikali tunajali maslahi yao," alisema Ulega.

Naye Besta alimhakikisha Waziri Ulega kuwa TANROADS itaendelea kusimamia makandarasi kwa karibu ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati.

"Tutaendelea kufanya hivi (kusimamia makandarasi kufanya kazi usiku na mchana). Hata pale ambapo Waziri wa Ujenzi hautakuja kufanya ziara za kushtukiza, tutahakikisha kazi inaendelea kwa kasi ili kufanikisha lengo la kupunguza msongamano wa magari jijini Dar es Salaam," alisema.

Meneja wa Mradi wa BRT, Allen Natai, alisema kuwa kazi ya kujenga miundombinu ya barabara za mabasi yaendayo haraka inaendelea vizuri.

Ziara ya Waziri Ulega imeonesha dhamira ya serikali ya kuhakikisha miradi mikubwa ya maendeleo inakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa ili kuboresha huduma kwa wananchi. Alisema ziara hiyo pia imetoa msukumo mpya kwa utekelezaji miradi ya miundombinu ya BRT jijini Dar es Salaam.



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mwanza, Mrakibu wa Polisi (SP) Sunday Ibrahim (kushoto), akitoa elimu na kuwakumbusha kanuni za usafirishaji madereva wa mabasi yaendayo mikoani pamoja na wasaidizi wao alipofanya ukaguzi wa kushtukiza jana katika eneo la Usagara uliolenga kudhibiti ajali zinaotokana na uzembe wa madereva. **PICHA: PETER ADOLPH**

# Polisi yashangazwa bodaboda kupiga picha ajali badala ya kuwaokoa walimu

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma limetoa ufafanuzi kuhusu ajali ya gari lililowaka moto na kusababisha vifo vya watu sita, wakiwamo dereva Vicent Milinga na mkewe Judith Nyoni, mwalimu wa Shule ya Msingi Lumalu, wilayani Nyasa.

Hii ni ajali iliyohusisha gari aina ya Toyota Prado lenye namba T 647 CVR ambalo juzi liligonga gema na kupinduka kisha kuwaka moto na kusababisha vifo vya watu sita, wakiwamo walimu wanne wa shule moja.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake mjini Songea, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya alisema ajali hiyo ilitokea saa 1:15 asubuhi katika kijiji cha Buluma, wilayani Mbinga kwenye barabara inayotoka Mbinga kwenda Mbambabay, eneo la kona za Chunya.

Kamanda Chilya alisema kuwa dereva wa gari hilo alifanikiwa kukata kona ya kwanza na alipofika kwenye kona ya pili, gari lilimshinda, likaacha njia na kugonga gema kisha linaingia mtaroni ambako liliwaka moto.

Kamanda Chilya alifafanuwa zaidi kuwa chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi uliosababisha dereva kushindwa kulimudu gari, hata likagonga kwenye gema na baadaye kupinduka huku likiwa linaelekea kwenye mtaro.

"Baada ya hapo cheche za moto zilianza kutoka na moto ukawaka na kuwateketeza wote waliomo katika gari hiyo," alisema kamanda huyo.

Hata hivyo, Kamanda Chilya alieleza kuwa kwenye eneo la tukio, wamebaini alikuwapo mwendesha bodaboda ambaye jina lake halijafahamika; mara tu baada ya ajali kutokea, alianza kupiga picha na abiria waliokuwamo katika gari walikuwa wanapiga kelele kwa ishara ya kuomba msaada.

"Huyu mwendesha bodaboda angeweza kuchukua jiwe na kuvunja vioo vya gari hilo ili waweze kutoka, lakini aliendelea kupiga picha ambazo amezisambaza kwenye mitandao," alisema.

Kamanda huyo aliwataja watu wengine waliofariki dunia kutokana na ajali hiyo kuwa ni Damas Nambombe, Dominika Ndau, John Mtuhi ambao wote ni walimu wa Shule ya Msingi Lumalu na Bonifasi Mapunda ambaye ni mfamasia.

Kamanda Chilya alisema mabaki ya miili yao yamechukuliwa na kupelekwa katika hospitali ya serikali wilayani Mbinga ambako ndugu wa marehemu watakabidhiwa baada ya kukamilika kwa uchunguzi wa vina saba unaohusisha Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Alionya watu wenye tabia ya kupiga picha matukio ya ajali na kuzisambaza kwenye mitandao, akisisitiza wananchi waache tabia ya kujifanya wao ni waandishi wa habari.

"Wawaachie wenye taaluma yao kwani nguvu iliyotumika kupiga picha kwenye tukio hilo ndio ilipaswa itumike kuokoa watu kwenye ajali hiyo," Kamanda Chilya alionya.

Pia aliwataka madereva katika msimu huu wa sikukuu wawe makini kwa kufuata sheria za usalama barabarani ambazo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matukio ya ajali.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customer-relations@guardian.co.tz***






Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, SACP Augustino Senga, akionesha mifuko 125 ya mbolea iliyofungashwa bila kibali iliyokamatwa katika mtaa wa Unyamwanga, Kata ya Tunduma wilayani Momba mwishoni mwa wiki. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Watiwa mbaroni kwa tuhuma kusafirisha vipodozi hatari wakitumia lori la mafuta

**Na Mwandishi Wetu,** SONGWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe limeendelea kufanya misako na doria katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo, likikamata watu wanne kwa tuhuma za kuingiza vipodozi vilivyopigwa marufuku nchini kutokana na kuwa viambata vya sumu.

Pia wamo wanaotuhumiwa kufanya udanganyifu katika uuzaji mbolea ya ruzuku.

Katika misako hiyo, jeshi hilo linamshikilia dereva wa lori la mafuta, Jackson Kashebo (45), mkazi wa Mbagala, mkoani Dar es Saalam aliyekuwa anaendesha gari lenye namba za usajili T 747 DDE na tela namba T 330 CJX aina Ya FAW TANK, mali ya KISMA TRANSPORT COMPANY LIMITED pamoja na msaidizi wake (utingo), William Sichone (34), mkazi wa mtaa wa Chapwa, wilayani Momba kwa tuhuma ya kusafirisha vipodozi vyenye viambata vya sumu aina mbalimbali maboksi 201.

Watuhumiwa hao walikamatwa juzi Desemba 28 asubuhi huko mtaa wa Keseria, kata ya Chapwa, wilayani Momba baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa za siri na kuweka mtego uliofanikisha kuwatia mbaroni watuhumiwa wakiwa wamepakia na kusafirisha shehena ya vipodozi vyenye viambata vya sumu maboksi 201. Inadaiwa shehena hiyo ilikuwa katika vyumba vya kubebea mafuta aina ya petroli vya tangi hilo la lori wakitokea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (drc) na kuviingiza nchini.

Vipodozi walivyokamatwa ni: Extra Clair maboksi 30, Betasol tube maboksi 14, Pawpaw cream maboksi 64, Snail white maboksi 16, Prety white maboksi manane, Extra clair lemon maboksi 27, Bronz tone maboksi manane, Clear therapy maboksi 14, Perfect white maboksi manane, Cocopup water maboksi 12, Esapharm movete Pcs 230 na Esapharma lemonvate Pcs 160.

Jeshi hilo kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na Halmashauri ya Mji Tunduma, limewakamata watu wawili; Gosso Mussa (32) na Prisca Filipho Shembe (37), wote wakazi wa Songea Tunduma, wakituhumiwa kukutwa na mifuko 125 iliyofungashwa bila kibali ikiwa ni pamoja na kuuza mbolea nje ya bei elekezi na kufanya udanganyifu wa kuuza mbolea ya DAAP Plus ya kampuni ya Minjingu iliyofungashwa kwenye mifuko ya DAP ya kampuni ya FALCON ETG.

**Aidha, alisema kutokana na ongezeko la watu kila mwaka serikali imeamua kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya kuwapatia wananchi kwa njia ya kuuza au kukodisha.**

Pia wanadaiwa kukutwa na mashine ya kushonea mifuko hiyo ambayo ni 'potable bag sealing machine' pamoja na mifuko tupu mipya 153 ya kampuni mbili tofauti.

"Tukio hili lilitokea Desemba 28, 2024 saa mbili asubuhi huko mtaa wa Unyamwanga, kata ya Tunduma wilayani Momba na kuikuta mifuko hiyo imefichwa kwenye ghala la kuhifadhia bidhaa mbalimbali za pembejeo kwa lengo ya kuiuza.

"Upelelezi wa shauri hili unaendelea na watuhumiwa wote wanne watafikishwa mahakamani pindi upelelezi utakapokamilika," inasomeka taarifa ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe iliyotolewa na SACP Augustino Senga, Kamanda wa Polisi mkoani humo.

Alisema jeshi hilo linatoa wito kwa jamii kuachana na biashara haramu za magendo, usafirishaji na uingizaji bidhaa zilizopigwa marufuku nchini kwa kuwa zinasababisha madhara kiafya kwa watumiaji.

Kamanda Senga alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe limeendelea kuwahakikishia wananchi kuwa lipo makini na imara katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao, na halitasita kumkamata mtu yeyote atakayebainika kujihusisha na uhalifu.

## Wastaafu 13,000 walipwa mafao kwa kikokotoo kilichoboreshwa

**Na Ashton Balaigwa**, MOROGORO

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) unaendelea kutekeleza agizo la serikali ulipaji mafao kwa kutumia utaratibu wa kikokotoo kilichoboreshwa.

Uongozi wa mfumo huo umesema kuwa tayari Sh. bilioni 126 zimelipwa kwa wastaafu 13,167 kuanzia Julai Mosi hadi kufikia Desemba mwaka huu.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa PSSSF, Yessaya Mwakifulefule alisema hayo wakati wa mafunzo na utoaji elimu kuhusu mfuko huo kwa waandishi wa habari ambao ni wanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Morogoro.

Mwakifulefule alisema mfuko ulianza kulipa mafao kwa wastaafu kuanzia Septemba mwaka huu kwa mujibu wa tamko la serikali lililotolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Alisema utekelezaji wa utoaji malipo hayo umekuwa wa aina mbili; asilimia mbili ambayo inalipwa moja kwa moja na mfuko huo na kuna malipo ya asilimia saba ambayo yanalipwa na serikali (mwajiri).

Alisema katika malipo ya asilimia mbili, kuna wale waliostaafu kwa mujibu wa sheria kuanzia Julai Mosi 2024, hao wameingia katika sheria mpya ambayo imeboreshwa bungeni.

Mwakifulefule alisema kundi hilo walilipwa jumla ya wastaafu 983 hadi kufikia Desemba mwaka huu, lakini pia wale wa asilimia saba walilipwa wastaafu 1,984 ambapo katika kipengele hicho mfuko umewalipa wastaafu 2,967.

Alifafanua kuwa ukiacha hao, pia kuna wale ambao walikuwa wanalalamikia mapunjo ambao walilipwa kwa mujibu wa sheria ya kikokotoo kilichokuwapo mwaka 2022.

Meneja huyo alisema kuwa hao nao walishalipwa kwa viwango vinavyoridhisha kwa maana baada ya kuboreshwa kwa sheria ya kikokotoo kipya.

Alisema PSSSF ililazimia kurejea tangu walipostaafu na kuanza kuwalipa mapunjo yao na katika kundi hilo waliolipwa na mfuko ni 3,364 ambao ni asilimia mbili na malipo yao ambapo wale wa asilimia saba kutoka serikalini walikuwa ni 9,803.

Meneja huyo alisema kuwa katika kundi hilo palikuwa na jumla ya wastaafu 13,167 na katika eneo hilo, mfuko umelipa jumla ya Sh. bilioni 126 kwa wastaafu wa makundi hayo mawili.

Meneja wa PSSSF Kanda ya Mashariki, Zaida Mahava, alisema kutokana na maboresho makubwa ya huduma yaliyofanyika kwa ngazi ya kanda, malalamiko yamepungua kwa kiasi kikubwa.

"Kwa sasa tumefikia sehemu nzuri kwa kuwa tumepunguza kero, tumepunguza malalamiko na hili ndilo lengo letu kuu kuhakikisha kwamba tunahudumia wanachama vizuri na kwa wakati," alisema Mahava.

Alisema kuwa katika uboreshaji utoaji wa huduma, PSSSF inaendelea kutoa elimu na mafunzo ya namna ya kutumia mfumo wa PSSSF Kidigitali kwa wanachama wake husani walioko maeneo ya vijijini.

Mahava alisema mafunzo hayo ambayo ni endelevu, yataendelea kutolewa ili kuyafikia makundi yote bila kumwacha mtu yeyote nyuma kwenye falsafa ya PSSSF Kiganjani.

Awali, Mwenyekiti wa MoroPC, Nickson Mkilanya alipongeza PSSSF kwa kuandaa fursa ya mafunzo kwa waandishi wa habari wa mkoa huo, akisema kuwa wako tayari kushirikiana katika kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu huduma zinazopatikana na kutolewa na mfuko huo nchini.

# Watiwa mbaroni kwa tuhuma za mauaji

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi mkoani Kagera linawashikilia watuhumiwa wawili wanaodaiwa kumuua Editha Andeson (32), mkazi wa Kilimahewa, Manispaa ya Bukoba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda jana aliwataja watuhumiwa hao ni Mtalemwa Answali na Kenedi Mganyizi, wote wakazi wa Kashenye, kata ya Kashai, Manispaa ya Bukoba.

Kamanda Chatanda alisema watuhumiwa wote waliokamatwa, wanadaiwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke huyo.

"Watu hawa walifanya kitu ambacho kimsingi ni cha kijinga, Edither alikuwa na mume ambaye ni bodaboda. Isivyo bahati, akawa na uhusiano wa kimapenzi na mtu mwingine ambaye walikuwa wanafanya kazi sehemu moja.

"Kwahiyo yule waliyekuwa wanafanya naye kazi sehemu moja, akaingiwa na wivu baada ya kuona ameanzisha tena uhusiano wa kimapenzi na mtu mwingine, yaani hawa wote wawili ni wezi, lakini kwa sababu ameanzisha mapenzi na mwizi mwingine, roho ikauma," alisema Kamanda Chatanda.

Alidai watuhumiwa hao walimuua mwanamke huyo kwa kutumia kamba ya mtandio.

Kamanda Chatanda alisema: "Baada ya kuingiwa na wivu, siku ya tukio, akamwita huyo mwanamke sehemu ambayo kwake aliona itakuwa rahisi kufanya tukio. Mara nyingi walikuwa wakikutana.

"Akamkaba kwa kutumia mtandio halafu wakashirikiana na mwenzake kumtoa katika eneo hilo na kwenda kumweka katika eneo lingine ili asitambulike kirahisi.

"Chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa mapenzi. Wakiwa katika uhusiano huo, Answari Mutalemwa alibaini kuwa mpenzi wake huyo ana uhusiano na mtu mwingine," alisema Kamanda Chatanda.

Alisema kitendo hicho kilimchukiza na kwa kushirikiana na wenzake waliamua kumuua Editha Anderson na kuchukua simu yake ya mkononi ili isipatikane.

# Bashe awataka viongozi kampuni ununuzi tumbaku wajisalimishe

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amewataka viongozi wa ngazi za juu wa kampuni inayonunua tumbaku katika mikoa ya Katavi, Shinyanga na Tabora, wajisalimishe katika kamati ya uchunguzi kujibu tuhuma zinazowahusishwa nazo za uhujumu uchumi.

> **"Majafa yalikamatwa yakiwa yamefichwa kwa ajili ya kuwauzia tena wakulima kinyume cha taratibu, walipaswa wapewe wakulima kwa kuwa ni mali yao," alisema Bashe.**

Viongozi hao wanadaiwa kuwauzia wafanyabiashara magunia ya kufungashia tumbaku badala ya kuyarejesha kwa wakulima ambao ndiyo wamiliki halali wa magunia hayo yanayoitwa "majafa".

Bashe alitoa agizo hilo juzi mjini Tabora wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya operesheni maalumu aliyoanzisha ya kuwasaka wanaofanya biashara haramu ya magunia hayo katika mikoa hiyo.

Pasipo kutaja kampuni hiyo, Bashe alisema kupitia operesheni hiyo, watu 15 wamekamatwa wakiwamo wafanyabiashara, wakihusishwa na majafa hayo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.8 ambayo yalitakiwa kurejeshwa kwa wakulima ili kufungia tumbaku ya msimu huu wa kilimo.

"Majafa yalikamatwa yakiwa yamefichwa kwa ajili ya kuwauzia tena wakulima kinyume cha taratibu, walipaswa wapewe wakulima kwa kuwa ni mali yao," alisema Bashe.

Waziri huyo alitangaza vita dhidi ya vitendo vya uhujumu uchumi vinavyofanyika kwenye zao hilo la tumbaku.

Bashe alisema: "Kuna mtandao mkubwa wa watu wanaojihusisha na vitendo hivyo nchini, kwahiyo ninapoanzisha operesheni hii watu wasiingilie kwa kuwa operesheni hizi zimekuwa zinaingiliwa na mambo ya kisiasa kwa sababu huenda ni wanufaika wakubwa wa vitendo hivi vya uhujumu uchumi kwenye zao hili la tumbaku."

Alisema wakulima hao wa tumbaku wamekuwa wanakatwa fedha kila mwaka katika msimu wa kilimo kulipia vifungashio vya majafa na kuwasababishia utitiri wa madeni, wajanja wachache wakiendelea kunufaika huku wakulima wakiendelea kukabiliwa na umaskini.

# JKCI yazidi kupanua huduma zake

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imefungua tawi jipya ikiwa ni kituo cha nne cha tiba Dar es Salaam kwa taasisi hiyo, ikilenga kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma za matibabu karibu na wanakoishi.

Kituo kikuu cha matibabu hayo ni JKCI-Upanga. Sasa taasisi hiyo ina vituo vingine vya JKCI-Dar Group; JKCI-Kawe (Mkapa Health Plaza) pamoja na JKCI-Oyster Plaza, vyote vikiwa mkoani Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam kwenye ufunguzi wa tawi la JKCI-Oyster Plaza.

Alisema taasisi hiyo imekuwa inawafikia wananchi waliko pamoja na mikoani, kuwapa huduma bobezi za uchunguzi na matibabu ya moyo.

Alisema tawi la JKCI-Oyster Plaza lilianza kutoa huduma bobezi za moyo mwishoni mwa wiki, lengo likiwa kuwapa fursa wananchi kupata huduma katika maeneo tofauti na kupunguza msongamano ulioko katika makao makuu ya taasisi, Upanga.

"Tumekuwa tunawafuata wananchi mikoani kuwapa huduma sasa tumeamua kuanzisha matawi ya taasisi, hii pia ni sehemu ya kuwafuata wananchi mahali walipo.

"Hapa tulipo leo (juzi), tunawapa nafasi wananchi wa eneo hili kupata huduma karibu, lakini pia hata wale wanaotoka mbali tunawapa nafasi, ili kupunguza msongamano ulioko makao makuu," alisema Dk. Kisenge.

Bingwa huyo wa magonjwa ya moyo alisema JKCI pia inaendelea kuyafikia makundi ya watu mbalimbali kuwapa huduma za uchunguzi na matibabu ya moyo, ili yote yawe mabalozi wazuri kwa wenzao na kuwa na tabia za kuchunguza afya zao mara kwa mara.

"Tumekuwa tukiwafikia watu tofauti kuwafanyia uchunguzi wa magonjwa ya moyo, kipindi hiki cha kufunga mwaka tunatoa huduma kwa wasanii na wanamichezo kila Jumamosi na Jumapili katika kliniki yetu ya Kawe, wanahabari tulishawapa huduma hii huko nyuma ila tutakuja kuwarudia tena," alisema.

Alitoa wito kwa wasanii na wanamichezo kuendelea kujitokeza kufanya uchunguzi wa magonjwa ya moyo, akisema kinga ni bora kuliko tiba na kama watagundulika mapema watakuwa kwenye nafasi ya kutibiwa magonjwa hayo mapema na kupona.

Miongoni mwa wananchi waliofika katika tawi hilo jipya, ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema huduma za afya zikiwa karibu na jamii, zinatoa motisha kwa jamii kufika hospitalini na kufanya uchunguzi wa afya, hivyo kupunguza matumizi ya dawa yasiyo sahihi.

"Mara nyingi tumekuwa tukipata hali za maumivu ama kuumwa kichwa, mafua, kikohozi, kifua tunaenda duka la dawa kununua dawa tu bila ya kufanya uchunguzi, lakini kama tutakuwa karibu na hospitali itatusaidia kwenda kupima kwanza na kupata ushauri wa daktari kabla ya kununua dawa," alisema.

Msimamizi wa kliniki JKCI-Oyster Plaza, Nyanjura Nyaruga, alisema kliniki hiyo imeanza kwa kuwa na mwitikio mkubwa wa watu waliofika kupata huduma za uchunguzi na matibabu ya moyo.

Nyanjura ambaye ni Ofisa Muuguzi Mbobezi wa Magonjwa ya Moyo, alisema katika kliniki hiyo wanatoa huduma za kliniki ya moyo; kliniki ya mishipa ya damu; kliniki ya magonjwa ya moyo kwa watoto; huduma za maabara, huduma za mazoezi (fiziotherapia) kwa wagonjwa wa moyo na huduma za dharura.

"Wananchi wasisite kufika katika kliniki yetu hii kwani tumejipanga kufikisha huduma bora kwenu na tutakuwa tukitoa huduma zetu kwa muda wa saa 24," alisema Nyanjura.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA IRINGA, MBEYA NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Dodoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi 02 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Ijumaa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi Alhamisi tarehe 02 Januari, 2025.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua Namba 3 (Tume Huru ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

**Limetolewa tarehe 19 Desemba, 2024 na:**

**Saida Hilal Mohammed**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218302902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga kazichezeni mechi hizi CAF kama fainali

**WIKI** ijayo wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Simba na Yanga zinarejea tena kwenye anga hizo kucheza michezo ya raundi ya nne ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Mabingwa wa Tanzania Bara Yanga, watakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Januari 4, mwakani, kucheza na TP Mazembe baada ya mechi iliyopita timu hizo kutoka sare ya bao 1-1 nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Simba inayoiwakilisha nchi kwenye mechi za Kombe la Shirikisho Afrika, itasafiri kwenda ugenini kupambana na CS Sfaxien ya Tunisia kwenye mchezo wa raundi nne hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Ukitazama msimamo wa makundi hayo ya A, katika michuano yote ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, inaonesha mechi zinazofuata ni muhimu zaidi kwa wawakilishi hao wa Tanzania na zitakiwa kupata ushindi ili kujiweka vema huko mbele kama zinataka kwenda hatua ya robo fainali.

Yanga inayoshika nafasi ya mwisho kwenye Kundi A Ligi ya Mabingwa, ikiwa na pointi moja, inatakiwa ipate ushindi, iwe mvua ama jua ili kuweka hai matumaini ya kusonga mbele.

Mpaka sasa Yanga haijashinda mchezo wowote, ikitoka sare moja na kupoteza miwili, hivyo inahitaji ushindi ili angalau kuwa na pointi nne kwa ajili ya kuinua matumaini yao.

Ushindi wowote dhidi ya TP Mazembe utawapa morali, wachezaji, viongozi na mashabiki wa timu hiyo wa kupambana na michezo miwili iliyobaki ugenini dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan na nyumbani kwa Mpaka dhidi ya MC Alger ya Algeria.

Kufungwa au sare Januari 4, mwakani nyumbani kutawafanya kunyong'onyea na matumaini ya kusonga mbele yataanza kufifia.

Kwa maana hiyo, viongozi wa Yanga wanatakiwa kuiandaaa timu kana kwamba inakwenda kucheza fainali. Wachezaji nao wanatakiwa kuingia uwanjani kwa kupambana na kupigania nembo ya klabu yao, huku mashabiki wakifanya kazi yao ya kuwashangilia na kuwatia moyo wachezaji wao mwanzo mwisho wa mchezo.

Kwa upande wa Simba itashuka dimbani kwenye Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi, Januari 5, mwakani, kucheza dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia baada ya mchezo uliopita kushinda nyumbani kwa mabao 2-1.

Kundi A hilo la Simba limekaa kimtego mno kwani Wanamsimbazi hao, CS Constantine na Bravo do Maquis zote zina pointi sita. Hivyo Simba inatakiwa kwenda kushinda mchezo huo ugenini, na kama ikishindikana kabisa basi kupata angalau sare, lakini si kupoteza.

Nayo inatakiwa icheze kama inacheza mchezo wa fainali ambao ukimalizika dakika 90. Ushindi wowote ule utaifanya kufikisha pointi tisa na hapo itahitaji alama moja tu ili kujihakikishia nafasi ya kufuzu robo fainali.

Kwa bahati nzuri inacheza na timu ambayo haina alama hata moja, huku zile zingine ambazo nazo zina pointi sita, zitakuwa zikipambana zenyewe kwa zenyewe. Hii ni faida kwa Simba. Kama moja itafungwa itabaki hapo hapo na pointi sita. Lakini kama zitatoka sare zitakuwa na pointi saba kila moja na hii yote itakuwa faida kwa Simba kama itashinda.

Tayari Simba ina faida ya kwenda kucheza mechi dhidi ya wapinzani wao hao bila kuwa na mashabiki. Hivyo wachezaji wa Simba ambao wana uzoefu wa kucheza ugenini mbele ya mashabiki tena kwa timu za Afrika Kaskazini, kwenda kucheza bila mashabiki kwao tunaamini ni nusu ya ushindi.

Simba haitakiwi kupoteza mechi hii, badala yake iicheze kimkakati kwani kupoteza kutaifanya kujiweka kwenye mazingira magumu licha ya kwamba itakuwa imebakisha michezo miwili.

Ushindi kwa wenyeji wao hao utaamsha ari yao ya kupambana na kuwa na kuongeza ari yao ya kwenda kushinda michezo miwili iliyobaki, hivyo kulifanya kundi kubwa gumu zaidi, hivyo ni wakati kwa Simba na Yanga kupambana kufa kupona.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# 2025 uwe wa mafanikio sekta ya michezo, vyama viige TFF

Na Adam Fungamwango

**WALA** si siri kuwa hakuna taasisi yoyote ya michezo Tanzania iliyofanya vizuri nchini kwa mwaka 2024 kama Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF).

Wakati vyama vingine vikisuasua, vingine vikijikongoja na vingine vikijitahidi kuelekea kwenye mlengo sahihi, TFF imekuwa kinara kwa vitendo.

Mbali na timu zake za mpira miguu, Simba na Yanga kutinga hatua za makundi, Yanga ikiwa Ligi ya Mabingwa na Simba Kombe la Shirikisho Afrika, lakini imefanikisha timu zake saba za taifa kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika.

Hivi karibuni, Timu ya Taifa ya soka ya Vijana chini ya miaka 17, Serengeti Boys, ilifanikiwa kufuzu kucheza fainali za AFCON chini ya miaka hiyo zitakazofanyika nchini Morocco mwakani.

Hii ni baada ya kuichapa, Sudan Kusini mabao 4-0, katika mchezo wa kusaka kucheza fainali hizo kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki (CECAFA).

Pia mwaka huu ilifuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Walemavu (BAFCON), zilizofanyika mwaka huu huu nchini Misri.

Kikosi cha Timu ya Taifa chini ya miaka 15 nacho kilifanikiwa kufuzu fainali za shule barani Afrika, huku Tanzania ikiwa mwenyeji.

Timu ya Taifa chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes, nayo haikuwa nyuma, kwani ilifuzu fainali za AFCON, ambazo zinatarajiwa kuchezwa nchini Ivory Coast.

**Timu ya Taifa chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes, nayo haikuwa nyuma, kwani ilifuzu fainali za AFCON, ambazo zinatarajiwa kuchezwa nchini Ivory Coast.**

Kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars, nacho mwaka huu kilifanikiwa kukata tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (WAFCON), zinazotarajiwa kuchezwa nchini Morocco.

Kama vile haitoshi Tanzania imepeleka fainali timu mbili za soka wanaume, moja ya Wachezaji wa Ndani ya nchi na nyingine ni ya jumla.

CHAN, michuano ya wachezaji wa ndani, Stars ilifuzu fainali hizo zinazotarajiwa kupigwa mwakani katika nchi tatu za Tanzania, Kenya na Uganda.

Taifa Stars, timu kubwa ya soka Tanzania yenye wachezaji wote wa ndani na nje, yenyewe imefuzu (AFCON), zinazotarajiwa kuchezwa mwakani nchini Morocco.

Shukurani kwa rais TFF, Wallace Karia na uongozi wake kwa kuyafanya yote haya, na amekua na mwendelezo wa kufanya vizuri mwaka hadi mwaka.

Naishauri TFF kutobweteka na sifa pamoja na maendeleo hayo, badala yake kuhakikisha inafanya zaidi ya ilichokifanya kwa mwaka 2025.

Mfano kwa sasa Tanzania ni moja kati ya nchi zitakazokuwa mwenyeji wa fainali za CHAN, hivyo yanatakiwa maandalizi kabambe ya kukisuka kikosi imara ambacho kitaweka rekodi nyingine ya kufanya vema kwa mwaka 2025.

Natumai pia kama vikosi vyote zilivyotinga fainali hizo vitaandaliwa na kufanya vizuri, inawezekana mwishoni mwa mwaka 2025 Tanzania ikaweza rekodi ya aina yake kubwa na nzuri zaidi kwenye soka.

Kabla sijamaliza napenda kuvishauri vyama na mashirikisho mengine ya michezo kuiga mfano kwa TFF. Ikiwezekana hata kwenda kuomba siri au mikakati inayofanywa kiasi cha kufanikiwa kwa sababu vyote viko chini ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

Baadhi ya vyama vya michezo vimekuwa na matatizo mengi yanayofanya kutofanya vizuri na wanamichezo wao kulalamika mara kwa mara.

Nadhani umefika wakati sasa vyama vingine vyote kuiga kinachofanywa na TFF kwa maendeleo ya michezo yote Tanzania.

MAKALA

# Vigogo walioingilia zabuni ya bil. 9.8/- NCAA na kusababisha hasara wachukuliwe hatua

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA utata uliibuliwa mwanzoni mwa mwaka huu kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii kuingilia zabuni yenye thamani ya Sh. bilioni 9.80 katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Uamuzi wa wizara hiyo kuingilia zabuni hiyo umeripotiwa kusababisha hasara ya zaidi ya Sh. milioni 700. Hata hivyo, hadi sasa, ikiwa ni zaidi ya miezi minane tangu kuripotiwa kwa suala hili, hakuna mtendaji wa serikali aliyewajibishwa kutokana na hasara hiyo.

Hoja hiyo imo katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23 ambamo anabainisha kuwa kitendo cha wizara kuingilia mchakato wa ununuzi NCAA kimesababisha ongezeko la gharama kwa Sh. milioni 702.68.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka 2022/23, CAG anasema NCAA ilikuwa na zabuni Na. EA/055/2020-2021/HQ/W/01 kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka hiyo.

Kwa mujibu wa CAG, hiyo ni zabuni iliyotolewa tarehe 09 Machi 2022 kwa gharama ya mkataba ya Sh. bilioni 9.80 baada ya taratibu za tathmini.

Hata hivyo, CAG anaeleza kuwa amebaini kwamba, mnamo tarehe 21 Aprili 2022, zabuni hiyo ilifutwa kwa kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mdhibiti anasema kuwa, wizara tajwa ilielekeza NCAA kufuta na kutangaza upya zabuni hiyo. Kutokana na maelekezo hayo, zabuni ilitangazwa tena tarehe 06 Mei 2022, na mzabuni huyo huyo aliyetangazwa mshindi awali, alipewa tena mkataba, safari hii ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 10.48.

Hiyo ina maana kwamba, mkataba mpya ulikuwa juu zaidi kwa Sh. milioni 686.60 huku CAG akibainisha kuwapo gharama nyingine za mchakato wa pili wa zabuni, Sh. milioni 16.08.

"Ni maoni yangu kuwa, hapakuwa na mantiki ya kufutwa kwa zabuni hiyo awali," CAG anasema katika ripoti yake hiyo na kuongeza kwamba:

"Kwa mujibu wa Kanuni ya 231 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 75 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2016, iwapo kulikuwa na malalamiko yoyote kuhusu uteuzi wa mzabuni aliyeshinda katika mchakato wa zabuni, wazabuni ambao hawakufanikiwa walitakiwa kutoa malalamiko ama kwa kuyapeleka kwa Ofisa Masuuli wakati wa muda wa kusubiri au kwa kukata rufani kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na si vinginevyo.

"Hali hii inachangiwa na ukiukwaji Sheria ya Ununuzi wa Umma na kutofuatwa kwa taratibu, jambo lililosababisha ongezeko la bei ya mkataba na kuchelewesha utekelezaji wa ujenzi."

Kutokana na hali hiyo, CAG anapendekeza NCAA na Wizara ya Maliasili na Utalii kuzingatia matakwa ya sheria na taratibu za ununuzi ili kuepusha gharama ambazo si za lazima na kusaidia ufikiwaji malengo ya Mamlaka.

CAG pia anapendekeza serikali inapaswa kubaini iwapo hasara hiyo ilisababishwa na uzembe au kushindwa kutekeleza majukumu ipasavyo kinyume cha Kifungu cha 2(c) cha Sheria ya Kukusanya Madeni kutoka kwa Maofisa wa Serikali ya Mwaka 1970 kwa ajili ya kurejesha hasara hiyo kutoka kwa maofisa husika.



CAG Charles Kichere

Kuagiza zabuni ifutwe na kutangazwa upya kisha kutunuku zabuni hiyo kwa mzabuni yuleyule aliyeshinda awali, kunaibua shaka kuhusu uadilifu wa waliotoa uamuzi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, ambaye ni CAG mstaafu (2006-2014), anasema kuwa Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, kinamtaka CAG akibaini viashiria vya rushwa wakati wa ukaguzi, aarifu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhusu viasharia alivyobaini ili vichunguzwe hata kabla ya Ripoti ya CAG kukabidhiwa kwa mamlaka husika.

Joseph Mwaiswelo, Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma TAKUKURU, anathibitisha CAG alitekeleza matakwa hayo ya kisheria wakati anakagua hesabu za NCAA kwa mwaka 2022/23.

Baada ya kubaini utata katika zabuni hiyo ya NCAA, Mwaiswelo anasema CAG alitoa taarifa kwa TAKUKURU. Suala hilo ni miongoni mwa yanayochunguzwa na taasisi hiyo.

Kama ilivyodokezwa awali, kufuta zabuni kisha kutunuku kwa mzabuni yuleyule aliyeshinda awali huku malipo ya mkataba yakiongezwa, kunaibuka shaka dhidi ya uadilifu wa watendaji hao wa serikali.

Ni muhimu mamlaka husika kuchukua hatua dhidi ya watendaji hao ili kutoa fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo au wenye nia ya kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, hivyo kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa mali ya umma.

Leo ni mwana na miezi sita tangu TAKUKURU ipewe taarifa na CAG kuhusu kuwapo viashiria vya rushwa katika kuingilia zabuni hiyo, lakini hakuna aliyechukuliwa hatua na taasisi hiyo kuhusiana na suala hili.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Jengo la Makao Makuu ya NCAA

MAKALA

# Serikali irejeshe mabilioni iliyochukua NHIF

Na Mwandishi Wetu



UHAI wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeanza kuimarika baada ya kuripotiwa kuwa mfuko huo ulikuwa hatarini kufisilika.

Hiyo ilitokana na waajiri kutowasilishi kwa wakati michango ya wanachama wa mfuko; serikali kutolipa mabilioni ya shilingi iliyokopa kwenye mfuko; wastaafu kulipiwa matibabu bila kuchangia; huku magonjwa yasiyo ya kuambukiza yakigharimu mfuko mabilioni ya shilingi kila mwaka.

Kifungu cha 9 cha Sheria ya Mfuko huo kinawataka waajiri waliosajiliwa kuwasilisha michango inayodaiwa kwa mwezi husika ndani ya siku 30 baada ya mwisho wa mwezi.

Hata hivyo, inaporejewa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2022/23, mnaripotiwa kuwa jumla ya michango iliyokuwa inadaiwa hadi kufika tarehe 30 Juni 2023 ilikuwa Sh. bilioni 42.57.

Kati yake, michango ambayo zinadaiwa taasisi za serikali ni Sh. bilioni 19.04 sawa na asilimia 45 na Sh. bilioni 23.53 sawa na asilimia 55 zinajumuisha madeni kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali.

Uchambuzi zaidi wa CAG kuhusu hesabu za NHIF umebaini kuwa, kati ya michango yote ya wanachama inayodaiwa na mfuko huo, michango ya Sh. bilioni 19.6 sawa na asilimia 40 inadaiwa zaidi ya siku 30.

Vilevile, mfuko ulikusanya Sh. bilioni 5.34 ya madeni hadi kufikia mwishoni mwa Novemba 2023 na kuacha deni linalodaiwa la Sh. bilioni 11.56.

Kwa mujibu wa CAG, sababu kuu zinazochangia madeni ya muda mrefu ya michango inayodaiwa kutoka mashirika ya umma, ni urasimu katika kuthibitisha madeni.

Ni hali inayosababisha kuwa na mkusanyiko wa madeni ya muda mrefu kutoka mashirika ya umma, jambo ambalo linaathiri hali ya kifedha ya NHIF.

Madeni ya muda mrefu pia yanasababisha changamoto za ukwasi katika mfuko, hivyo kuathiri shughuli za mfuko, ikiwa ni pamoja na kushindwa kuwalipa watoa huduma kwa wakati.

Katika hili, CAG anapendekeza; serikali ihakiki malimbikizo ya michango iliyobaki na kuidhinisha kwa ajili ya malipo; na mfuko uendelee kufuatilia madeni ambayo hayajalipwa na kuhakikisha kiasi chote kinakusanywa.

Hata inapotazamwa hali ya uhimilivu wa NHIF, CAG anabainisha kuwa mfuko huo umekuwa ukipata hasara kwa miaka mitano iliyopita.

Mdhibiti anabainisha kuwa mfuko umepata hasara ya Sh. bilioni 156.77 kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikiwa ni uimarikaji kutoka hasara iliyopatikana mwaka wa fedha 2021/22 ya Sh. bilioni 205.95.

Ukaguzi wa hesabu za mfuko umebaini kuwa michango ya wanachama kwa mwaka wa fedha 2022/23 iliongezeka kwa asilimia 14.6 kutoka Sh. bilioni 552.58 mwaka 2021/22 mpaka Sh. bilioni 633.51 mwaka wa fedha 2022/23.

Ni ongezeko kubwa kulinganishwa na ongezeko la matumizi ya wanachama ya asilimia 10.2 kutoka Sh. bilioni 674.25 mwaka 2021/22 hadi Sh. bilioni 743.28 mwaka wa fedha 2022/23.

Ripoti ya ukaguzi wa hesabu za mfuko inaonesha hasara kutokana na kuhudumia wanachama ilipungua kutoka Sh. bilioni 121.67 mwaka 2021/22 hadi Sh. bilioni 109.77 mwaka 2022/23.

"Hii inaashiria kuimarika kutoka mwaka wa fedha 2021/22 ambapo ongezeko la michango ya wanachama lilikuwa asilimia 12.9 kutoka Sh. bilioni 489.48 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 552.58 mwaka wa fedha 2021/22, ikiwa ni kidogo kulinganisha na ongezeko la matumizi ya wanachama la asilimia 24.6 kutoka Sh. bilioni 540.55 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 674.25 mwaka wa fedha 2021/22," CAG anafafanua.

**KIINI CHA TATIZO**

CAG anataja mambo makubwa manne yanayoathiri uhai wa muda mrefu wa NHIF, yakijumuisha mikopo ya serikali ambayo haijalipwa.

Kwa mujibu wa CAG, mikopo ambayo haijalipwa ni ya Sh. bilioni 208 anayoitaja inasababisha mzigo mkubwa wa kifedha, na hivyo kupunguza uwezo wa mfuko kuwekeza katika huduma muhimu na miundombinu.

Hata hivyo, CAG anasema amepewa taarifa kwamba, serikali kupitia Wizara ya Fedha imepanga kulipa Sh. bilioni 180.03 (bila riba na adhabu) katika Bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha (2024/25).

Jambo la pili linalonyooshewa kidole kuhatarisha uhai wa NHIF, ni wastaafu kunufaika bila kuchangia, ikielezwa kuwa mfuko unagharamia matibabu ya wastaafu na wenza wao ambao hawachangii mfuko.



Waziri wa Afya, Jenista Mhagama

Ni hali ambayo CAG anaitaja inadhoofisha mfuko kwa sababu matumizi ya wastani ya kundi hili ni Sh. bilioni 84.70 kwa mwaka. Hata hivyo, uongozi wa juu wa NHIF umeshatolea ufafanuzi hoja hii, ukieleza kuwa jambo hili ni la kisheria; mtumishi wa umma anapaswa kuhudumiwa na mfuko hata anapostaafu utumishi serikalini.

Jambo la tatu ni kuongezeka magonjwa yasiyo ya kuambukiza, CAG akifafanua kuwa kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa wanachama, kunadhoofisha mfuko kwa kiasi kikubwa kwa kuwa matumizi ya wastani kwa kundi hili ni Sh. bilioni 137.80 kwa mwaka.

CAG anataja jambo la nne ni uchaguzi wa wanachama walio na wagonjwa, akifafanua kuwa wanachama wa hiari kwa makundi fulani, hasa kutoka sekta binafsi zilizo rasmi na zisizo rasmi, hujiunga na mfuko pale tu wanapohitaji matibabu ya gharama kubwa, hali inayodhoofisha mfuko.

Kwa ujumla, CAG anasema hasara endelevu kutokana na kuhudumia wanachama na hasara ya mfuko kwa ujumla inaathiri uimara na uendelevu wa mfuko.

Hivyo, ni muhimu uongozi wa NHIF ufikirie upya mikakati ya namna ya kuzalisha faida kutokana na kushughulika na wanachama na faida ya jumla kwa miaka mingi kwa uendelevu wa mfuko na serikali ilipe mkopo inaodaiwa.







# Wanaharakati watoa angalizo matukio ukatili Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WANAHARAKATI wametoa tahadhari kwa wakazi wa miji ya Moshi, Hai, Siha na Rombo kuhusu matukio ya ukatili wa kingono, ubakaji na ulawiti wakati huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Wamesema miji hiyo kwa sasa imefurika maelfu ya watu wanaokwenda kwenye makazi yao ya asili kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na mwanaharakati anayepambana na ukatili wa kijinsia mkoani humo, Veronica Ollomi, akiwataka wazazi/walezi, kujitahidi kutupia macho suala zima la ulinzi wa watoto katika sikukuu hizo.

Alikuwa akizungumza juzi na viongozi wapya wa serikali za mitaa na vijiji wa Wilaya ya Moshi, waliokuwa wakinolewa kupitia mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT).

Mafunzo hayo yanahusu masuala ya jinsia na namna wanavyoweza kutumia nafasi zao kusimamia haki na usawa wa kijinsia katika maeneo yao.

"Sisi kama wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia, tunapenda kutoa wito kwa jamii kusherehekea sikukuu hizi kwa amani na utulivu lakini pia kujitahidi katika suala zima la ulinzi wa watoto.

"Kwa sababu watoto ndiyo mara nyingi waathirika wakubwa wa masuala ya ukatili wa kijinsia, ikiwamo ubakaji, ulawiti. Inawezekana matumizi ya vilevi kupita kiasi vinaweza kusababisha mtu akapata ushawishi wa kumbaka mtoto au kumlawiti mtoto.

...Kwa hiyo tunaomba jamii isherehekee sawa sikukuu vizuri lakini pia wahakikishe kama wazazi, kwa sababu kuna kawaida watoto kuruhusiwa kutoka kwenda kutembea, hebu wazazi wahakikishe ulinzi wa watoto wao ili waendelee kuwa salama na kuhakikisha kwamba unajua mwanao anakwenda wapi.

Zaidi alifafanua: "Kama unamwachia kwenda kutembea hakikisha unajua mahali anapokwenda kutembea, kwa sababu dunia ya sasa hivi siyo salama, watoto wengi hawako salama. Kwa hiyo tunaomba sana wazazi wazingatie hilo ili tumalize mwaka vizuri na mwakani watoto waweze kuendelea na masomo yao kama kawaida."

Kwa mujibu wa Veronica, maeneo mengi ya starehe, wazazi na walezi wengine wanakwenda na watoto, kitu ambacho kisheria hakiruhusiwi.

Mwanaharakati kutoka Kata ya Mwika Kusini, Easther Temba alieleza namna wakazi wa kata hiyo, wanavyostaajabishwa na kuchukizwa na kitendo cha wazazi, kumwachia mtoto anayesoma darasa la awali (jina limehifadhiwa) kuzurura katika maeneo ya starehe na kurudi nyumbani kati ya saa 5 mpaka saa 6 usiku.

# Samia awajaza 'manoti' madereva bodaboda Arusha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametoa Sh. milioni 10 kwa uongozi wa Chama cha Waendesha Bodaboda Wilaya ya Arusha, kwa ajili ya kuwawezesha kukamilisha utaratibu wa kuanzisha chama cha ushirika.

Licha ya kutoa kiasi hicho pia amewapa pikipiki mbili kwa chama hicho, zitakazotumiwa na viongozi wa chama ngazi ya wilaya na mkoa kwa shughuli ya kuwatembelea wanachama wao kusikiliza changamoto zinazowakabili na kuzitatua.

Fedha hizo zimekabidhia jana (leo) jijini Arusha na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Mohamed Ali Kawaida, wakati wa mkutano mkuu wa Umoja wa Waendesha Bodaboda Wilaya ya Arusha, uliombatana na uzinduzi wa mfumo wa kidijitali wa utambuzi wa wanachama wao.

Aidha, alisema Rais Samia amefikia uamuzi wa kutoa Sh.milioni 10 kwa kuwa awali waendesha bodaboda hao walikosa fedha za ukamilishwaji utaratibu wa kuanzisha ushirika huo.

Pia, kiongozi huyo ameliagiza Jeshi la Polisi kwa kushirikia na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU), kufanya uchunguzi wa kupotea kwa fedha zaidi ya Sh.milioni 200 zinazodaiwa kuchukuliwa na baadhi ya viongozi wa chama hicho waliomaliza muda wao.

Vilevile aliwataka waendesha bodaboda kujisimamia wenyewe na kuacha kufanya matukio yasiyofaa ikiwamo kutotumia dawa za kulevya na kunywa pombe kupita kiasi wakati wakitekeleza majukumu yao.

Kadhali, alilitaka kundi hilo kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa watu wanaotumia mwamvuli wa bodaboda na kuvunja sheria.

**Vilevile aliwataka waendesha bodaboda kujisimamia wenyewe na kuacha kufanya matukio yasiyofaa ikiwamo kutotumia dawa za kulevya na kunywa pombe**

"Zingatieni sheria za usalama barabarani, lakini pia msijiingize kwenye dawa za kulevya kwa kutumia mwaya wa bodaboda kwa kufanya uhalifu toeni taarifa na ushirikiano kwa Jeshi la Polisi," alisema.

Katika hatua nyingine waendesha bodaboda hao wameiomba serikali kupunguza gharama za ukataji wa leseni ya udereva kufikia Sh.30,000 kwa kuwa hadi mchakato kukamilika unawagharimu Sh.99,000 ili kila mmoja aweze kumiliki leseni.

Naye Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, alitoa Sh.milioni 10 kuchagia mfuko wa chama hicho.

Akiwasilisha malalamiko kwa Mjumbe wa Kamati Kuu, Gambo alisikitishwa kwa wahusika wanaodaiwa kuchukua na kutafuna fedha hizo Sh.milioni 200 za umoja huo, kutokukamatwa hadi sasa ikiwa imepita miaka minne.

Gambo alitumia fursa hiyo kumwomba Kawaida kumsaidia kupeleka malalamiko hayo kwa Rais Samia ili atumie vyombo vyake vya dola kuwakamata wahusika walioiba fedha hizo, huku akiahidi donge nono la Shilingi milioni moja kwa yoyote atakayesaidia kutoa taarifa za wahusika wanapopatikana.

Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda Wilaya ya Arusha, Shwaibu Hamisi, alisema wilayani humo wana bodaboda 12,500 huku mkoa huo ukiwa na bodaboda 26,000.

Mwenyekiti wa Bodaboda na Bajaji Taifa, Said Chenja, alisema kazi ya bodaboda siyo ya laana na alimshukuru Rais Samia kwa kuwapunguzia faini kutoka Sh.30,000 hadi kufikia Sh.10,000.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Arusha, Dk. Wilfred Solilel, alitoa rai kwa wasafirishaji hao kuwa makini barabarani na kuacha kuvunja sheria.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (mwenye shati la mistari), akikagua maonesho ya bidhaa mbalimbali za asili kutoka Mkoa wa Kilimanjaro zikiwamo zinazotengenezwa kwa miti, majani, mbegu, mizizi na migomba na dawa za asili katika tamasha la asili la kiutamaduni la Kilimanjaro Cultural Festival KCF mwishoni mwa wiki. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Prof. Mkenda awaambia Rombo waanzishe benki

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

WAKATI Umoja wa Wanarombo (RU) wanaoishi ndani na nje ya Tanzania wakichangishana zaidi ya Sh. milioni 242.3 ili kujijenga kijamii na kiuchumi ikiwamo kugharamia misiba, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, amewataka wafikiri juu ya uanzishaji wa Benki ya Wananchi wa Rombo.

Hadi kufikia Desemba 27 mwaka huu, RU iliyoanzishwa miezi 20 iliyopita, licha ya kugharamia shughuli 44 za mazishi, ilikuwa imewekeza Sh. milioni 70 kwenye UTT AMIS (Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi Rasilimali Tanzania).

Akizungumza katika mkutano wa kwanza wa RU uliofanyika juzi Mashati, Kata ya Katangara Mrere, wilayani hapa, Prof. Mkenda, alisema wakazi hao wanajukumu la kuangalia mkakati wa kujiendeleza mmoja mmoja na kujenga mikakati, ambayo itawaendeleza wote kwa pamoja.

"Ndiyo maana umoja kama huu, ni jukwaa zuri sana la kwenda mbali zaidi. Sisi tuna ushirika mkubwa sana kwenye mazishi, tuna ushirika mkubwa sana kwenye harusi na ni muhimu sana yote mawili.

"Mtu akipoteza mpendwa wake anahitaji watu wamkimbilie wamsaidie na umoja huu ni njia mojawapo. Tunashika mkono kuhakikisha kwamba tutakaa tutafurahi na kuwabariki. Lakini sasa ni lazima tuangalie hatua moja mbele zaidi.

Huu umoja wetu tulionao katika kushikana mkono wakati wa majanga, mazishi, harusi; tuanze sasa kufikiria tunaangalia mitaji ya biashara, tunaangalia huduma za afya, tunaangalia juhudi mbalimbali za kuleta maendeleo.

...Ni kitu kikubwa kuwekeza, mnachokifanya ninyi sasa hivi kudunduliza lakini kuwekeza na kuangalia fursa ni muhimu sana. Kilichobaki kikubwa zaidi ni kuangalia kipi kitatusaidia."

Katibu Mkuu wa RU, Anthony Kawishe, alisema umoja huo ulianzishwa Mei mwaka 2023 kutokana na wana Rombo wengi kuwa kwenye mahangaiko ya kukabiliana na changamoto zao kadhaa, hasa za msiba pindi inapojitokeza.

Kwa mujibu wa Kawishe, RU, imejengwa kwa mfumo wa kitaasisi na siyo kama mali ya wachache kutokana na namna inavyofanya kazi na kujiendesha kwake.

"Malengo yetu ni kufanya mageuzi makubwa ya kijamii na kiuchumi na kufikia lengo la kuwa taasisi kubwa ya kuigwa ndani na nje ya Rombo katika nyanja za kiuchumi na kijamii," alisema.





# Tisa mbaroni kuendesha gari wakiwa wamelewa

**Na Restuta Damian,**
KAGERA

JESHI la Polisi mkoani Kagera limewafungia leseni madereva tisa kwa makosa ya kuendesha gari wakiwa wamelewa pamoja na mwendokasi barabarani.

Taarifa za kukamatwa kwa madereva hao zilitolewa juzi na Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Blasius Chatanda wakati akizungumza na waandishi wa habari kufuatia doria mbalimbali walizozifanya barabarani.

"Magari yameongezeka sana na abiria wamekuwa wengi wanakuja na kwenda kusalimia na kujumuika na ndugu zao kusherehekea kwa pamoja, hivyo doria zetu zimejikita kwenye udhibiti wa madereva wanaokiuka sheria na kanuni za usalama barabarani," alisema Chatanda.

Aidha, alitaja madereva hao kuwa ni pamoja na Frank Samwel, Hashim Kitwe, Rajab Mwenda, Eden Tarimo, Gerald Suluba, Aizack Henrico, Idd Ramadhan, Focus Bernad, Wilfred Rwegasira.

Katika hatua nyingine Kamanda Chatanda alisema Jeshi la Polisi limewakamata watuhumiwa wawili wa mauaji ya Editha Anderson (32) mkazi wa Kata ya Kashai Manispaa ya Bukoba mkoani hapa.

**"Chanzo cha mauaji hayo kikiwa ni wivu wa mapenzi wakiwa katika mahusiano hayo ambapo Answari Mutalemwa alibaini kuwa mpenzi wake huyo...**

Alisema watuhumiwa hao ni Answari Mutalemwa (25) mkazi wa Kata ya Kashai, Kennedy Muganyizi (25) ambao wote walikuwa na mashine ya kimapenzi na marehemu ambako wanatuhumiwa kutekeleza mauaji hayo Desemba 12, 2024.

"Chanzo cha mauaji hayo kikiwa ni wivu wa mapenzi wakiwa katika mahusiano hayo ambapo Answari Mutalemwa alibaini kuwa mpenzi wake huyo anauhusiano na mtu mwingine.

Alisema kitendo hicho kilimchukiza na kwa kushirikiana na wenzake waliamua kumuua Editha Anderson na kuchukua simu yake ya mkononi ili isipatikane.

Kadhalika alisema Jeshi la Polisi limewakamata watu wawili wakiwa na mashine saba za kuendesha boti kati yake tano ni aina ya Yahama, marina, Suzuki na nyavu 184.

Alisema kati ya boti hizo moja yenye namba TZBBKZ 2014 MV IMANI imetambuliwa na raia wa nchini Uganda na kwamba boti hiyo iliibiwa nchini humo kisha kuletwa nchini huku ikibadilishwa rangi.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro (katikati), akikabidhi mbuzi, chakula na vinywaji kwa watoto wenye ulemavu mbalimbali ambao wanaishi kituo cha Buhangija Shinyanga kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Mwaka Mpya 2025, zawadi ambazo zimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wanawake Nyahanga waongoza kudai taraka

**Na Marco Maduhu,**
KAHAMA

MWENYEKITI wa Baraza la Usuluhishi wa Kata ya Nyahanga mkoani Mara, George Simba, amesema eneo hilo linaongoza kwa kuwa na kesi za wanawake kuomba taraka.

Alibainisha hayo jana kwenye mdahalo wa kujadili matukio ya vitendo vya ukatili ndani ya jamii na kutafuta suluhisho, ulioandaliwa na Shirika la Help Age Tanzania, kupitia mradi wa chaguo langu haki yangu kwa ufadhili wa Serikali ya Finland kupitia Shirika la UNFPA.

"Kumeibuka wimbi la wanawake kudai taraka katika baraza letu la usuluhishi hapa Nyahanga, chanzo ni migogoro ya kiuchumi hasa kwa wanawake ambao wanafanya shughuli zao, wakipata fedha kidogo wanaona waume zao hawafai na kutaka kuachana ili wajitawale," alisema Simba.

Alisema wamekuwa wakiwashauri wanawake hao na kusuluhisha jambo hilo kwa kuwapatia elimu, kwamba mwanaume ndiyo nguzo ya familia, hata kama uchumi wake umeyumba na wao kuwa na pesa kuwazidi.

Alisema hali hiyo ni sehemu pia ya ukatili na unyanyapaa kwa wanaume ambao hawana kipato cha kuridhisha na kwamba hawapaswi kuachwa bali wavumiliane kwenye shida na raha, kama walivyoapa wakati wa kufunga ndoa.

Katibu wa Jukwaa la Wanawake wa Kata hiyo, Halima Hussein, alisema ukatili kwa wana ndoa bado upo, huku akitaja miongoni mwa sababu kuwa ni pamoja na mikwamo ya kiuchumi.

Alisema tatizo lingine wanawake wamekuwa wakipigwa na waume zao na hata kufukuzwa ndani ya nyumba, huku akitolea mfano kwa jirani yake ambaye alipigwa na mumewe na kufukuzwa.

Mmoja wa wazee wa kimila, Elizabeth Rubasha, alisema ukatili wa kijinsia kwa sasa umekuwa ukisababishwa na utandawazi, kwa watu kupenda kuiga mambo ya kigeni.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Ester Mkumbae, alisema ukatili wa kijisia bado upo kwa jamii japo siyo kwa kiwango kikubwa.

Alisema wamekuwa wakichukua hatua pamoja na kuendelea kutoa elimu wakishirikiana na mashirika.

Ofisa ufuatiliaji kutoka Shirika la Help Age, Winnie Hinaya, alisema wameendesha mdahalo huo kwa makundi rika mbalimbali, ili kubadilisha mitazamo hasi na kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii.

Alisema katika mdahalo huo wameshirikisha makundi rika yote wakiwamo vijana, wanawake, mabinti wazee, watu wenye ulemavu, viongozi wa dini, polisi kata, maofisa maendeleo na ustawi wa jamii.

# DC atoa maagizo kutokomeza utapiamlo

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Wilaya ya Igunga, Sauda Mtondoo amesema licha ya wilaya hiyo kujipanga kuongeza uzalishaji wa vyakula vyenye lishe ili kutokomeza utapiamlo, maofisa lishe wanapaswa kuja na mikakati ya muda mrefu kudhibiti tatizo hilo.

Alitoa agizo hilo juzi katika kikao cha wajumbe wa kamati ya lishe wilaya huku akiwataka wataalamu wa lishe kuongeza ubunifu utakaoleta matokeo chanya miongoni mwa jamii ikiwamo kuboreshwa afya zao.

Sauda alisema kamati hiyo ni muhimu kwa kuwa imebeba maslahi ya afya za wakazi wa wilaya hiyo, hivyo kuwataka kuja na mikakati chanya inayotekelezeka kwa manufaa ya wananchi.

Alibainisha kuwa moja ya mikakati ya halmashauri hiyo ni kuongeza uzalishaji wa chakula lishe ili kujenga afya za wananchi na kupunguza tatizo la utapiamlo na magonjwa yatokanayo na ukosefu wa lishe.

"Kikao hiki ni muhimu sana kwa kuwa kinajadili maslahi mapana ya jamii na afya zao, naamini bajeti itakayopitishwa itazingatia malengo ya halmashauri ya kuimarishwa suala zima la lishe miongoni mwa jamii," alisema.

Alifafanua kuwa huwezi kuzungumzia suala la uchumi au maendeleo kama afya za wananchi haziko vizuri na kubainisha kuwa afya inaanzia kwenye lishe bora.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Joseph Mafuru, alishauri wataalamu hao kuangalia uwezekano wa kutumia maeneo ya wazi yaliyo karibu na shule kuanzisha kilimo cha mazao lishe ikiwamo bustani za mboga.

"Maofisa elimu tusaidieni kubainisha maeneo yaliyo wazi karibu na shule ambayo yanafaa kuanzisha bustani za mboga na mazao mengine ili kuwezesha watoto wetu kupata chakula shuleni," alisema.

Mkuu wa Idara ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe katika halmashauri hiyo, Lucia Kafumu, alishauri maofisa lishe kuanzisha bustani za mboga na chakula lishe kingine, kuuza maziwa na kufuga kuku.

Aidha, aliwataka kuboresha mipango yao ili kuhakikisha changamoto za lishe zinazoikabili jamii katika wilaya hiyo zinatatuliwa na kuleta mafanikio chanya.

Nipashe
Spotika



WANAMICHEZO BORA WA KUANGALIWA MWAKA 2025 UK. 12




# WASHAMBULIAJI WA5 BORA EPL 2024/2025

**LONDON, England**

MASHABIKI wanaweza kuthamini wachezaji wanaozuia mabao yasiingie, lakini wale wanafunga ndio huuza tiketi.

Kwa bahati nzuri Ligi Kuu England ni nyumbani kwa watu hao ambao wanajua kabisa wavu uko wapi.

Kuwasili Erling Haaland kumevuka kile ambacho wengi waliwahi kufikiria kuwa kinawezekana na nyota huyo wa Norway amelithibitisha hilo.

Makala haya inawaangalia washambuliaji watano bora zaidi kwenye Ligi Kuu England msimu wa 2024/25.

**5. Bukayo Saka (Arsenal)**

Bukayo Saka anaendelea kuimarika zaidi Arsenal na bila shaka ndiye mchezaji wao muhimu zaidi.

Si tu kwamba Mwingereza huyo anafunga mabao mara kwa mara, lakini pia huwapa wachezaji wenzake vitu vingi na anacheza kwa akili ya soka zaidi ya miaka yake ya ujana.

Mwondoe Saka kutoka kwa timu ya Arsenal inakuwa dhahiri ni kiasi gani Mikel Arteta anamtegemea.

Acha tuone jinsi wiki chache zijazo zitakavyokuwa bila winga huyo akiwekwa nje kutokana na kufanyiwa upasuaji wa misuli ya paja.

**4. Luis Diaz (Liverpool)**

Kop alikuwa akimpenda Diaz tangu alipotikisa kule Porto katikati mwa msimu wa 2021/22. Alianza kwa ustadi mkubwa Anfield, lakini wakati mbio zake za kukimbia na nguvu nyingi zikiendelea kusifiwa, Mcolombia huyo aliiteka mioyo ya mashabiki.

Hata hivyo, Arne Slot imesaidia Diaz kufikia gia nyingine huku winga huyo akianza kuchanua katika nafasi ya namba tisa.

Anabakia kuwa mchezaji asiyechoka ambaye ndiye ufunguo wa mafanikio ya Liverpool.

Diaz pia amekuwa mmoja wa wachangiaji muhimu zaidi wa mabao kwa Liverpool.

**3. Chris Wood (Nottingham Forest)**

Chris Wood yuko kwenye msimu wake wa nane kama mchezaji wa Ligi Kuu England na katika kampeni tano kati ya hizo amefunga angalau mabao 10 au zaidi - rekodi ambayo hakuna anayeonekana kuizungumzia.

Hakika, hizo si namba za kushinda mataji, lakini zinaonesha jinsi Wood anavyofaa katika kiwango hiki.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa New Zealand anazichachafya safu za ulinzi kwenye ligi kutokana na utimamu wake na anaweza kuwa na mabao mengi zaidi mwishoni mwa msimu huu wa 2024/25.

**2. Alexander Isak (Newcastle United)**

Mshambuliaji huyo wa Newcastle United amekuwa fowadi aliye katika kiwango bora zaidi.

Isak alirekodi mabao manane katika mechi zake nne zilizopita za ligi, huku mabao yakifika kwenye hafla hiyo kuu dhidi ya Arsenal na Liverpool. Pia akashinda bao bora la mwezi uliopita.

Raia huyo wa Sweden amekuwa msaada mkubwa kwa Newcastle ambayo kwa sasa iko katikati ya msimamo.

**1. Mohamed Salah (Liverpool)**

Wakati Bukayo Saka anachanua kwa uwezo wa kufunga mabao, Mohamed Salah amekuwa kwenye kiwango hicho kwa miaka mingi.

Raia huyo wa Misri anapuuzwa na baadhi ya watu, lakini anabakia kuwa kielelezo cha Liverpool - ambayo ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kutwaa taji la Ligi Kuu msimu huu.

Kwa uchache zaidi, amewapita Jermain Defoe na Robbie Fowler katika orodha ya wafungaji mabao wa muda wote wa Ligi Kuu England na hivyo kuimarisha hadhi yake kama gwiji wa siku hizi.

## ISIKUPITE

PENALTI aliyokosa mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, wakati wakitoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Etihad dhidi ya Everton Alhamisi iliyopita, ni ya pili kwake kukosa kati ya penalti 17 ambazo ameshapiga kwenye ligi hiyo.



# WANAMICHEZO BORA WA KUANGALIWA MWAKA 2025



MBAPPE

**LONDON, England**

KALENDA ya michezo inapozidi kupamba moto kuelekea mwaka 2025, ulimwengu unatazamiwa kuona msururu wa matukio ya kusisimua na burudani za kila aina.

Kuanzia mashindano ya Riadha ya Dunia, Ndondi na Ligi Kuu ya England, kuna burudani kwa kila mtu.

Hii ni orodha ya wanamichezo wa kuangaliwa mwaka 2025, kuanzia kwenye mpira wa miguu, kikapu, riadha hadi ndondi, twende sasa...

**Lamine Yamal**

Mchezaji wa Barcelona na Hispania, Lamine Yamal ameshinda tuzo ya Golden Boy mwaka 2024.

Tuzo hiyo iliyoanzishwa na gazeti la Italia la Tuttosport, hutolewa kwa mchezaji bora wa Ulaya kwa wanaume chini ya umri wa miaka 21, huku waandishi wa habari wakipiga kura kwa kutumia mfumo wa pointi.

Yamal mwenye umri wa miaka 17, alijiimarisha katika kikosi cha kwanza cha Barcelona msimu uliopita kabla ya kuisaidia Hispania kushinda Euro 2024.

Winga huyo alifunga bao moja na kusaidia mengine manne huku akitajwa kuwa mchezaji chipukizi bora wa michuano hiyo.

Mnamo Oktoba, Yamal alishinda tuzo ya Kopa, zawadi sawa na iliyotolewa wakati wa sherehe ya Ballon d'Or ya 2024.

Yamal amefunga mabao sita na kutoa asisti nane katika mechi 16 za mashindano yote msimu huu.

**Faith Kipyegon**

Bingwa wa Dunia wa Michezo ya Olimpiki kwenye Riadha, Faith Kipyegon, alikuwa na msimu mzuri mwaka 2023 aliposhinda mbio zake na kuweka rekodi tatu za dunia.

Kipyegon alivunja rekodi za dunia katika mbio za mita 1,500, 5,000 na kushinda mara mbili medali ya dhahabu ya mbio za mita 1,500 na 5,000 kwenye mashindano ya Dunia.

Pia alipata tuzo ya Mwanariadha Bora wa Kike wa 2023.

Kuelekea 2025, Kipyegon anapendelea zaidi kushinda medali za dhahabu katika mbio za mita 1,500 na kuna matumaini kwamba rekodi zaidi atazifikia.

**Noah Lyles**

Noah Lyles ni mwanariadha wa Marekani ambaye alijulikana kama "mtu mwenye kasi zaidi duniani" baada ya kushinda medali tatu za dhahabu katika mita 100, mita 200, na Relay ya mita 4 × 100 kwenye mashindano ya dunia ya mwaka 2023.

Lyles pia alishinda mbio za mita 100 kwa wanaume kwenye Michezo ya Olimpiki ya 2024, akimshinda Kishane Thompson wa Jamaica.

**Kylian Mbappe**

Kiwango cha mshambuliaji wa Real Madrid, Kylian Mbappe "kiko chini kwa sasa" lakini ana dhamira ya kuvuka kipindi kigumu, kwa mujibu wa kocha wake, Carlo Ancelotti.

Fowadi huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25, ambaye alijiunga na Real kwa uhamisho wa bila malipo kutoka Paris St-Germain Julai, mwaka huu, amekuwa na wakati mgumu tangu alipowasili pale kwenye dimba la Bernabeu.

"Mbappe yuko chini kama kila mtu mwingine, lakini ana ari ya kumaliza kipindi hiki," alisema bosi wa Real, Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari.

"Tatizo alilonalo ni la kila mtu. Unaweza kumwelekeza Vinicius Junior], Rodrygo au Jude Bellingham. Ni wakati mgumu kwa kila mtu."

Mchezaji huyo anatarajiwa kuimarika zaidi mwaka 2025 wakati ambapo atakuwa amefahamiana vizuri kimchezo na wachezaji wenzake wa Real Madrid.

**Beatrice Chebet**

Beatrice Chebet ni mwanariadha wa Kenya wa mbio ndefu ambaye ndiye anayeshikilia rekodi ya dunia katika mbio za mita 10,000 na medali ya dhahabu katika michezo ya Olimpiki ya 2024 katika mbio za mita 5000 na 10,000, mbali na kuwa mwanamke wa tatu katika historia kushinda mbio mbili tofauti kwenye michezo ya Olimpiki.

Mwaka 2022, Chebet alishinda medali za dhahabu katika mbio za mita 5000 kwenye michezo ya Jumuiya ya Madola, mashindano ya Afrika, na Ligi ya Diamond na medali ya fedha katika mbio za mita 5000 kwenye mashindano ya Dunia. Chebet pia alishinda medali za dhahabu katika mashindano ya Dunia ya 2023 na 2024.

Katika mashindano ya vijana, Chebet alishinda medali za dhahabu katika mbio za mita 5000 kwenye mashindano ya Dunia chini ya umri wa miaka 20 ya IAAF 2018 na sehemu ya Wanawake ya Vijana ya Mashindano ya Dunia ya Mbio za Nyika za 2019.

**Gervonta Davis**

Gervonta Bryant Davis anayejulikana pia kwa jina lake la utani 'Tank', ni bondia wa Marekani. Ameshikilia taji la WBA uzito mwepesi tangu 2023. Pia alishikilia taji la Shirikisho la Ndondi la Kimataifa (IBF) mwaka 2017, taji la WBA super featherweight mara mbili kati ya 2018 na 2020, na taji la WBA la uzito mwepesi mwaka 2021.

Kufikia Mei 2024, Davis aliorodheshwa kama mchezaji wa pili bora zaidi duniani katika uzani mwepesi na ESPN.

Bondia huyo ana mpango wa kustaafu mwaka 2025, na kuacha historia ambayo imewashangaza mashabiki wengi.

**Victor Wembanyama**

Nyota wa timu ya mpira wa kikapu ya Marekani, San Antonio Spurs, Victor Wembanyama ameshinda tuzo ya mchezaji bora anayechipukia wa NBA mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ndiye Mfaransa wa kwanza kushinda tuzo hiyo baada ya kuwa na wastani wa pointi 21.4

Wembanyama, alipata kura zote 99 za nafasi ya kwanza.

**Letsile Tebogo**

Letsile Tebogo ni mwanariadha kutoka Botswana. Alishinda medali ya dhahabu katika Olimpiki ya 2024 kwenye mashindano ya mbio za mita 200, na ushindi wake uliipatia Botswana dhahabu ya kwanza ya Olimpiki.

Pia alishinda medali ya fedha katika mashindano ya Dunia ya 2023 katika mbio za mita 100 na kufuatiwa na medali ya shaba katika mbio za mita 200 siku tano baadaye.

Tebogo alishinda katika mbio za mita 100 na kushika nafasi ya pili kwenye mbio za mita 200 katika mashindano yote mawili ya Riadha ya Dunia ya 2021 na 2022. Mwaka 2021, alikua mwanariadha wa kwanza wa Botswana kushinda taji la mita 100 katika kiwango chochote cha ubingwa wa Dunia.

Yeye ndiye bingwa wa Afrika wa mita 200 mwaka 2022 na kuwa mshindi mwenye umri mdogo zaidi wa taji hili katika historia ya mashindano. Alishinda tuzo ya mwanamichezo bora wa dunia upande wa wanaume 2024.

**Amos Serem**

Mwanariadha Mkenya Amos Serem alisitisha mfululizo wa ushindi wa miaka miwili wa ubingwa wa Olimpiki, Soufiane El Bakkali na kushinda taji lake la kwanza la Ligi ya Diamond la mbio za mita 3000 kuruka viunzi kwenye fainali ya Allianz Memorial van Damme - Wanda Diamond League mjini Brussels nchini Ubelgiji.

Serem alimzidi El Bakkali kwa urahisi katika awamu ya mwisho na kushinda kwa saa 8:06.90. El bakali wa Morocco alimaliza katika nafasi ya pili kwa muda wa 8:08.60 huku Mohamed Amin Jhinaoui wa Tunisia (8:09.68) akimaliza wa tatu.

**Daniel Dubois**

Daniel Dubois ni mwanamasumbwi mtaalam wa England. Ameshikilia taji la uzani mzito la Shirikisho la Ndondi za Kimataifa (IBF) tangu Juni 2024. Hapo awali, aliwahi kushikilia taji la uzito wa juu la Chama cha Ngumi cha Dunia (WBA) kutoka 2022 hadi 2023.

Akiwa mwanariadha, alikuwa bingwa mara tano wa England kwa upande wa vijana. Dubois anajulikana kwa uwezo wake wa ngumi nzito akishinda mara 21 kati ya 22 kwa njia ya knockout.

Ushindi wake mkubwa ni dhidi ya bingwa wa zamani wa uzani mzito zaidi duniani, Anthony Joshua.

**Faith Cherotich**

Faith Cherotich ni mwanariadha wa Kenya ambaye ni mtaalam wa mbio za mita 3000 za kuruka viunzi. Akiwa na umri wa miaka 17, alishinda tuzo ya shaba katika mashindano ya riadha ya Dunia ya walio chini ya umri wa miaka 20 ya 2021 yaliyoandaliwa Nairobi nchini Kenya.

## Nukuu

"Kinachonifurahisha katika kundi hili la wachezaji - tuna ubora wa kufanya kitu maalum. Jambo la muhimu zaidi ni kujitolea kunakohitajika kushinda kitu. Si lazima tujilinganishe na timu iliyopita. Lazima kundi hili tutengeneze historia yetu wenyewe msimu huu," **Kipa wa Liverpool, Alisson, hukusu nafasi ya klabu hiyo kwenye mbio za ubingwa Ligi Kuu England msimu huu.**



"Sitakata tamaa. Nataka kuwa hapa. Nataka kufanya hivyo na kwa hali tuliyo nayo, lazima tuifanye. Bila shaka nataka [kumaliza mwenendo mbaya], kila mtu anataka hilo. Sitaki kuwakatisha tamaa watu wangu katika suala la klabu, mashabiki, watu wanaoipenda klabu hii. Jaribio kubwa zaidi ni kurudi tena, lakini tumefanya hivyo hapo awali," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, kabla ya kuivaa Leicester City jana kwenye mechi ya Ligi Kuu England.**



"Unaweza kuhoji kuwa nimekuwa hapa kwa mwezi mmoja na nimekuwa na [awamu] nne za mazoezi, lakini hatushindi. Huo ndio ukweli. Ninajua kwamba ikiwa hatutashinda, bila kujali kama watalipa ununuzi au la, kila kocha yuko hatarini, ninapenda hiyo kwa sababu hiyo ndiyo kazi," **Kocha wa Manchester United, Ruben Amorim**



# MZUNGUKO WA KWANZA LIGI KUU BARA KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

MZUNGUKO wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara umemalizika kwa timu zote kucheza michezo 15 ya kwanza, huku chache zikiwa zimeshaanza kucheza mechi za mwanzo za mzunguko wa pili.

Hadi mzunguko huo unamalizika Simba iko kileleni, imemaliza mwaka 2024 ikiwa kwenye kilele cha msimamo na itaendelea kuwa hapo hadi Januari 20, mwakani, mechi za Ligi Kuu zitakapoendelea kwa mujibu wa ratiba.

Wakati Ligi Kuu ipo katikati, baadhi ya timu zimeweka rekodi na takwimu nzuri za kuvutia na zisizovutia.

Wachezaji nao hawapo nyuma, wamekuwa wakishindana kuweka rekodi nzuri ambazo zimewafanya waendelee kuzungumzwa na kuwa midomoni mwa mashabiki wa soka.

Katika makala haya, tunakuletea rekodi na takwimu mbalimbali za timu pamoja na wachezaji hadi kufikia mzunguko huo na kuziweka kwa mtindo wa namba...

**40#** Hizi ni pointi za Simba ilizokusanya hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, ikiwa imeshacheza michezo 15 ya mwanzo.

**36#** Ni dadi ya pointi za Azam FC, ilizokusanya mpaka sasa ikicheza michezo 16 na kukamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi.

**33#** Baada ya kufungwa bao 1-0 juzi kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida, timu ya Singida Black Stars ina idadi hii ya pointi, ikiwa kwenye nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi Kuu.

**31#** Namba hii inasimama kama idadi ya mabao ya kufunga ya Simba ambayo mpaka sasa ndiyo timu inayoongoza kwa kufunga mabao mengi kwenye ligi hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.



Kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', anayeongoza kwa 'asisti' nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, akiwa ametoa pasi tisa za mabao. **MPIGAPICHA WETU**

**29#** Timu ya KenGold imefungwa idadi hii ya mabao na kuwa timu inayoongoza kwa kuruhusu mabao mengi kwenye Ligi Kuu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

**25#** Namba hii ni idadi ya mabao iliyofunga Azam FC mpaka sasa kwenye ligi, ikiwa inashika nafasi ya tatu kwa timu iliyofunga mabao mengi kwenye ligi, baada ya Simba na Yanga.

**19#** Ni pointi za Mashujaa iliyo kwenye nafasi ya saba na JKT Tanzania iliyo kwenye nafasi ya nane.

**17#** Ni idadi ya pointi zinazomilikiwa na timu mbili. Coastal Union na Namungo zote zina pointi hizi kila moja, lakini Wanamangushi wanashika nafasi ya 10 na wenzao Namungo ya 11 kwenye msiamamo wa ligi.

13# Namba inayosimama kama idadi ya mechi za ushindi ambazo Simba imeshinda mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

**12#** Hizi ni 'clean sheets' za kipa wa Simba, Moussa Camara, akiwa ni golikipa anayeongoza kwa kukaa langoni bila kuruhusu wavu wake kuguswa.

**9#** Kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum anaongoza kwa kutoa pasi za mwisho za mabao kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, akiwa amefanya hivyo mara idadi hii.

**8#** Straika wa Singida Black Stars, Elvis Rupia, ndiye anaongoza kwa upachikaji mabao kwenye Ligi Kuu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, akiwa na idadi hii ya mabao.

**7#** Namba hii inasimama kama idadi ya mabao ambayo timu za Prisons na Pamba Jiji zimefunga. Ndizo timu zilizofunga mabao machache zaidi kwenye Ligi Kuu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza. Prisons inashika nafasi ya 13 na Pamba Jiji ya 14 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

**6#** Hizi ni pointi za KenGold, timu ambayo inashika mkia wa ligi mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

**5#** Ni idadi ya mabao ya Prince Dube kabla ya mchezo wa jana kati ya Yanga na Fountain Gate, lakini pia inasimama kuwa ni idadi ya 'asisti' za kiungo mshambuliaji wa Simba, Jean Ahoua, akifikisha idadi hiyo juzi kwenye mchezo dhidi ya Singida Black Stars.


**3#** Kipigo cha mabao 1-0 ilichokipata juzi dhidi ya Simba, kimeifanya Singida Black Stars kupoteza mechi mara idadi hii. Ilifungwa pia dhidi ya Yanga bao 1-0 na Azam mabao 2-0.

**2#** Ni idadi ya mechi ambazo Yanga na Azam zimepoteza kwenye ligi mpaka sasa, kabla ya Wanajangwani kushuka dimbani jana dhidi ya Fountain Gate.

**1#** Namba hii inasima kwa Simba ambayo imepoteza mechi moja na sare moja tu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu. Pia inaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu mpaka sasa.

**0#** Kabla ya mchezo wa jana wa Ligi Kuu kati yake dhidi ya Fountain Gate, Yanga ndiyo ilikuwa timu pekee ambayo haijatoka sare.

**JE, WAJUA?**



MANCHESTER City, ambayo imeshinda mataji sita kati ya saba yaliyopita ya Ligi Kuu England, imeshinda mechi moja tu kati ya 13 zilizopita za ligi hiyo na kupoteza tisa.



# Aliyepasuliwa uvimbe kichwani anaendelea vizuri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

AFYA ya Hussein Babu (18) mkazi wa Kijiji cha Boayi wilayani Babati mkoani Manyara, ambaye aliomba msaada kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kupatiwa matibabu ya uvimbe kichwani, inaendelea kuimarika katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH).

Kijana huyo ambaye amekuwa akisumbuliwa na tatizo la uvimbe kichwani tangu mwaka 2011, amefanyiwa upasuaji Desemba 26 mwaka huu na madaktari bingwa na wataalamu wa afya kutoka BMH, jijini Dodoma.

Mama mzazi wa Hussein, Aziza Said alisema tatizo hilo la uvimbe kichwani limemsumbua kijana wake tangu mwaka 2011 na baada ya kuhangaika kupata matibabu kwenye hospitali kadhaa hapa nchini bila mafanikio.

"Nililazimika kuomba msaada kwa Rais Samia baada ya kuona napitia changamoto za matibabu ya mtoto wangu, nashukuru sana kwa msaada tuliopatiwa hali ya kijana wangu inaendelea vizuri tofauti na alivyoletwa," alisema Aziza Said.

Aidha, aliwashukuru madaktari bingwa pamoja na wataalamu wa BMH kwa kufanikiwa kuondoa uvimbe kwa kijana wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Profesa Abel Makubi, alisema baada ya uongozi wa Mkoa wa Manyara kupata taarifa ya kijana huyo kuomba msaada wa matibabu kwa Rais kwa kushirikiana na idara ya afya ya mkoa huo, kijana huyo alifikishwa BMH Desemba 25, na kufanyiwa.

Alisema baada ya kufanyiwa vipimo na madaktari siku inayofuata alipelekwa katika chumba cha upasuaji kwa ajili ya kuendelea na matibabu chini ya uangalizi wa madaktari bingwa ambao walifanikisha zoezi hilo.

"Kwa sasa kijana Hussein yuko wodini akiendelea na matibabu chini ya uangalizi wa madaktari na wataalamu wa afya, hali yake inaendelea kuimarika tofauti na awali," alisema Profesa Makubi.

Alisema anaishukuru serikali kutokana na uwekezaji iliofanya katika sekta ya afya na BMH kwa ujumla vimewezesha jamii kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini kujitokeza kupata matibabu mbalimbali chini ya wataalamu wa afya.

Akielezea hali yake kijana Hussein Babu (18) alishukuru BMH kwa huduma ya matibabu aliyopewa, huku akisema hivi sasa anaendelea vizuri kiafya tofauti na ilivyokuwa awali na kuongeza kuwa anamshukuru Rais kwa kumpatia msaada wa matibabu.

Alisema afya yake ikiimarika ataendelea na majukumu yake ikiwamo kurudi shule kuendelea na masomo ambayo aliyakatisha kutokana na tatizo hilo lililomsumbua kwa muda mrefu.

# Samia kuongoza mamia ibada kuliombea taifa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajia kushiriki katika ibada ya mkesha wa kitaifa kwa ajili ya dua maalumu ya kuliombea taifa, Desemba 31, 2024 katika viwanja wa Nyerere Square Dodoma.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Fellowship of Churches (TFC), Dk. Godfrey Malasi, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ibada hiyo maalumu ya kumaliza mwaka.

Alibainisha kuwa viongozi wengine watakaoungana na Rais Samia kwenye ibada hiyo ni pamoja na wa madhehebu ya dini mbalimbali, siasa pamoja na waumini.

Dk. Malasi ambaye ni Mratibu Mkuu wa ibada zinazofanyika za mikesha ya kitaifa inayofanyika kila mwisho mwa mwaka alisema ni wakati wa kuungana kama taifa ili kuomba kwa sauti moja kwa ajili ya amani utulivu na ustawi wa Tanzania.

**Dk. Malasi ambaye ni Mratibu Mkuu wa ibada zinazofanyika za mikesha ya kitaifa inayofanyika kila mwisho mwa mwaka alisema ni wakati wa kuungana ...**

"Katika kitabu cha 1 Timotheo 2;1 kinasema kuwa "Basi kabla ya mambo nataka dua, sala, maombezi na shukrani zitolewe kwa ajili ya watu wote," alisema Askofu Malasi.

Pia, alisema dua na sala hiyo itakayofanyika italenga kutoa shukrani ya kitaifa kwa mwaka uliopita na kuomba baraka kwa mwaka mpya wa 2025 pamoja na kuombea maendeleo ya kiroho, kijamii na kiuchumi kwa taifa.

Alisema: "Niwaombe Watanzania tumalize mwaka kwa kushukuru na kufanya toba na tuanze mwaka mpya wa 2025 kwa maombi na baraka ambazo zitakazogusa maisha yetu na Taifa kwa ujumla".



Wananchi wa Kata ya Mnadani jijini Dodoma, wakifanya usafi wa mazingira kwenye maeneo yao ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya serikali ya kila Jumamosi ya ufanyaji usafi: **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Viongozi waliosoma Shule ya Mwenge wapanda miti

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JUMUIYA ya wanafunzi waliosoma Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida kuanzia mwaka 1991 hadi 1994 wamepanda miti 1,000 katika shule hiyo, ili kuunga mkono jitihada za serikali katika utunzaji wa mazingira.

Wanafunzi hao ambao baadhi hivi sasa ni wabunge, walimu, wahadhiri katika vyuo vikuu, madaktari, wahandisi, askari, viongozi wa dini, walipanda miti ya matunda ambayo itasaidia lishe kwa wanafunzi ambao bado wapo katika shule hiyo na miti ya kivuli kwa ajili ya kupumzikia.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Emmanuel Hanai, alisema suala la upandaji miti na utunzaji wa mapori ni muhimu sana kwani hivi sasa serikali inajihusisha na biashara ya kaboni.

"Tunatoa wito kwa Watanzania wote watunze mazingira hivi sasa suala la mazingira ni muhimu sana na hasa tukiangalia nguvu zinazofanywa na jumuiya za kimataifa katika mikutano mikubwa ya mazingira ambapo jitihada hizi ili ziweze kufanikiwa zianzie chini kwa wananchi," alisema.

Hanai, alisisitiza suala la utumiaji wa nishati safi kama ambavyo serikali imekuwa ikihamasisha na kuachana na matumizi ya nishati chafu ambayo imekuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira kutokana na kukatwa miti kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Naye Mbunge wa Iramba Mashariki, Francis Mtinga, alisema miti mingi imekuwa ikipandwa lakini inakufa na kwamba wakati sasa umefika miti iwe inapandwa kwa malengo.

Wakati wa maadhimisho ya 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara yaliyofanyika Desemba 9, 2024, Ofisa Maliasili Mkoa wa Singida, Charles Kidua alisema miti 13,399,031 ambayo ni kati 33,253,602 iliyopandwa katika Mkoa wa Singida katika kipindi cha kuanzia 2019 hadi 2024 imekufa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utunzaji hafifu.

"Katika uhifadhi wa misitu na mazingira mkoa umepanda miche 33,253.602 sawa na asilimia 63 ya lengo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na miti iliyopona ni 19,854,571 sawa na asilimia 59.7 ya miti iliyopandwa," alisema.

Kidua alisema sababu za miti mingi inayopandwa kufa ni kutokana na uharibifu unaofanywa na mifugo, utunzaji hafifu, mchwa kuharibu miche, kuwapo kwa vipindi virefu vya jua na uelewa mdogo wa wananchi juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Hata hivyo, alisema katika kuhifadhi mazingira mkoa umejiwekea dira na malengo kwa kuongeza utekelezaji wa upandaji miti kutoka asilimia 63 ya sasa mpaka asilimia 90 ifikapo mwaka 2030 na kuongeza idadi ya misitu ya hifadhi kufikia hekta 100,000 ifikapo mwaka 2030.





# Serikali yatangaza mabadiliko safari Mv Mbeya II

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI imeagiza meli ya abiria ya Mv Mbeya II inayofanya safari zake kati ya Bandari ya Kiwira wilayani Kyela mkoani Mbeya na Mbambabay mkoani Ruvuma kufanyika kila wiki.

Meli hiyo imekuwa ikifanya safari Kiwira- Mbambabay mara mbili kwa mwezi.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile alitoa agizo hilo alipofanya ziara katika Bandari ya Kiwira ambapo alisema meli hiyo itakuwa inatoka Bandari ya Kiwira kila Alhamisi na Kufika Mbambabay Ijumaa.

Vilevile alisema meli hiyo itaondoka Mbambabay kila siku ya Jumamosi na kufika Kyela Jumapili na kwamba lengo la serikali ni kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria katika ziwa hilo.

Alisema ratiba hiyo mpya itasaidia wananchi wanaoishi pembezoni mwa Ziwa Nyasa kunufaika na uwekezaji uliofanywa na serikali kwa kuhakikisha usafiri unaimarika ili wasafiri na kusafirisha bidhaa zao.

Alisema ratiba ya awali ilitokana na matatizo mbalimbali yaliyojitokeza ikiwamo kuongezeka kwa kina cha maji ndani ya ziwa hilo kulikosababisha kuanza kusuasua kwa safari ya meli ya abiria iliyolazimika kufanya safari mara mbili pekee kwa mwezi.

"Hapo katikati tulipata changamoto kubwa moja ya mabadiliko ya hali ya hewa, maji yalijaa na ikapelekea ratiba yetu kusuasua, sasa tumekubaliana ratiba hii haitakuwa mara mbili kwa mwezi tena itakuwa mara moja kwa kila wiki kama ilivyokuwa mwanzoni," alisema Kihenzile.

> **"Hapo katikati tulipata changamoto kubwa moja ya mabadiliko ya hali ya hewa, maji yalijaa na ikapelekea ratiba yetu kusuasua, sasa tumekubaliana ratiba hii haitakuwa mara mbili kwa mwezi tena itakuwa mara moja...**

"Na maagizo ninayoyatoa yasimamiwe kwa kuwa tunataka kuona wananchi wanaolizunguka Ziwa Nyasa wananufaika na rasilimali zilizopo hapa, tuone wananchi wanaosafiri kupitia Ziwa Nyasa wanafurahia uwekezaji uliofanywa na Rais Samia kwenye ziwa hili," aliongeza.

Alisema serikali imeshakubaliana na wabunge wa majimbo yanayozunguka Ziwa Nyasa pamoja na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kufanyia ukarabati mkubwa meli ya mizigo ya Mv Songea.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Mlagila alisema kurejeshwa kwa ratiba za meli kama ilivyokuwa awali itawasaidia wananchi kuwa na usafiri wa uhakika hasa wale wanaoishi kwenye maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo.

Alisema njia ya maji ndiyo njia inayowaunganisha wananchi wa Mkoa wa Mbeya na wa Mkoa wa Ruvuma hasa wilaya za pembezoni mwa ziwa hilo kwa bei rahisi zaidi.

"Ratiba hii itasaidia kuchochea hali ya uchumi kwa kuwa sasa wataweza kufanya shughuli za kibiashara kirahisi zaidi, bidhaa zinazosafirishwa kwa meli bei yake ni rahisi zaidi," alisema Mlaghila.

Naye Mbunge wa Jimbo la Ludewa mkoani Njombe, Joseph Kamonga alisema wananchi wa jimbo lake ni miongoni mwa wanufaika wa usafiri huo na kwamba wanaiomba serikali iiboreshe na meli ya mizigo ili ianze kufanya kazi.

Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Manga Gasaya alisema miongoni mwa matatizo yanayozikabili bandari zilizopo upande wa Wilaya ya Kyela ni pamoja na ubovu wa barabara. Alisema barabara hizo zinasababisha usafirishaji wa bidhaa na abiria kutoka Kyela kwenda katika bandari hizo kuwa mgumu na hivyo akaiomba serikali kuziboresha.



Koplo Hansi Ngolo, akizungumza na viongozi wa vitongoji, vijiji na kata ya Kwezitu wilayani Muheza jana, namna bora ya kupanga mikakati ya kuzuia uhalifu katika kipindi cha kuelekea mwisho wa mwaka. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# DC aagiza mafundi wazawa kupewa elimu ya ununuzi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Mbarak Batenga, ameagiza kufanyika kwa mafunzo kuhusu mfumo mpya wa kielektroniki wa manunuzi ya umma kwa mafundi wazawa na wafanyabiashara.

Aidha, amewaagiza viongozi wa vijiji na kata kuwaongoza na kuwasaidia mafundi wazawa na wananchi wenye uwezo wa kuwa wazabuni wa vifaa mbalimbali kujisajili kwenye mfumo huo, ili waweze kunufaika kwa kutoa huduma.

Alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki alipoongoza Kamati ya Usalama ya Wilaya kukagua ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika wilaya hiyo.

"Mafundi wote wazawa wapewe mafunzo na wasaidiwe kujisajili kwenye mfumo huo ili waweze kuomba na kutekeleza kazi mbalimbali za ujenzi wa miradi ya serikali kwenye maeneo yao wanayoishi," alisisitiza.

Alionya kamati za ujenzi kutopokea vifaa vyenye upungufu au vibovu kwa kuwa ndiyo chanzo cha miradi kukosa ubora.

Vilevile alisisitiza viongozi wa wilaya hiyo kuhakikisha wanaongeza usimamizi kwenye miradi hiyo ili itekelezwe kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa kulingana na thamani halisi ya fedha zilizotolewa na serikali.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Cuthbert Mwinuka alisema watayafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na kwamba kamati maalumu itapita kwenye kila mradi kutoa elimu ya namna ya kusimamia miradi inayotekelezwa.

# Mtendaji adaiwa kujinyonga kisa mazingira ya kazi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MTENDAJI wa Kijiji cha Mkwayungi mkoani Dodoma, Sikitu Mwasubila (31) amefariki dunia akidaiwa kujinyonga Mtaa wa Melinze katika Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamisha Msaidizi Mahamoud Banga aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema Sikitu alifika mkoani Njombe kumfuata mumewe ambaye ni mfanyabiashara kwa ajili ya kusherehekea sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya lakini Desemba 24, mwaka huu, siku moja kabla ya sikukuu anadaiwa alijinyonga.

Kamanda Banga alisema sababu za marehemu huyo kuchukua uamuzi wa kujinyonga ni kutokana na ugumu wa mazingira ya kazi huko alipokuwa katika Kijiji cha Mkwayungi kilichoko mkoani Dodoma.

"Alipata ajira hivi karibuni lakini mazingira ya kule yakawa yamemshinda na aliporejea hapa Njombe ambapo mume wake anaishi aliamua kuchukua maisha yake yeye mwenyewe kwa kisingizio hicho," alisema Banga. Alibainisha kwamba Sikitu aliacha ujumbe kuwa ndugu zake wamsamehe kwa maamuzi aliyochukua na muwe aendelee na maisha na mke ambaye ni mzazi mwenzie.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia Regan Sanga (24) mkazi wa Makambako kwa tuhuma za kuendesha genge la uhalifu lililokuwa likishiriki kwenye mauaji ya walinzi kwenye maeneo ya biashara, uporaji na uvunjaji.

Kamanda Banga alisema baada ya kukamatwa aliwaongoza askari na kufanikiwa kukamata vitu mbalimbali ambavyo alivipora kwenye matukio tofauti aliyoyafanya.

"Aliwaongoza askari na kufanikiwa kukamata vitu mbalimbali kama simu ndogo 25, simu janja tisa, betri za simu 11, flash 25, memory card saba, power bank mbili, laptop 1, CCTV kamera 2, saa ya ukutani na mashine ya kuhesabia fedha ambavyo alivipora katika matukio mbalimbali aliyoyafanya," alisema Banga.

Kamanda alisema Desemba 26, mwaka huu, majira ya saa tatu usiku wakati anakwenda kuonyesha mali zingine na walipojificha watuhumiwa wenzake alitoroka na kuanza kukimbia na hata askari walipopiga risasi hewani ili kumtahadharisha asikimbie lakini alikaidi na kuendelea kukimbia.

Alisema mtuhumiwa huyo alijeruhiwa na risasi mguu wa kushoto na kufanikiwa kumkamata ambapo kwasasa amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Njombe akiendelea na matibabu.

Alisema: "Mbali na kujihusisha na vitendo vya mauaji, ujambazi, uvunjaji wa kukata bati juu na kuingia ndani ya maduka mtuhumiwa huyo amehusika katika kuiba kwenye mikoa ya Njombe, Iringa, Songwe, Mbeya, Rukwa na Ruvuma."



## Serikali kujenga barabara za mijini, vijijini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali imejipanga kuimarisha miundombinu ikiwamo ujenzi wa barabara za mijini na vijijini, ili kuimarisha uchumi wa taifa.

Aliyasema hayo wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi Barabara ya Mazizini, Chukwani na Maungani yenye urefu (km 28.164).

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha kuwa maeneo yote yanayostahiki kupitiwa na miundombinu ya barabara zinajengwa kwa kiwango cha lami kwa lengo la kuwaondolea wananchi changamoto ya usafiri.

Alisema madhumuni makubwa ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwaweka huru wananchi wote bila ya kujali dini, rangi, kabila ama sehemu wanazotoka pamoja na kuwapatia maendeleo endelevu ambayo yatawasaidia katika kujikwamua kiuchumi.

Hemed alisema kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali atahakikisha wanayatangaza yale yote mema na mazuri yanayoendelea kufanyika nchini, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Aidha, aliwataka madereva na watumiaji wengine wa barabara kufuata sheria na miongozo ya usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizo za lazima zinazosababisha vifo, ulemavu wa kudumu na uharibifu wa miundombinu inayojengwa kwa gharama kubwa na serikali kwa maslahi ya wananchi wote.

Pia, alikemea tabia zinazofanywa na baadhi ya watu za kupandikiza chuki na matumizi ya lugha zisizo rasmi ambazo zitapelekea uvunjifu wa amani ambayo ndio tunu na faida kubwa ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964.

Pia, aliwataka wananchi kuendelea kuyatunza, kuyalinda na kuyatetea mapinduzi kwa maslahi ya vizazi vya sasa na baadaye.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhammed alisema serikali imedhamiria kuwaondolea wananchi wa Zanzibar changamoto ya usafiri kwa kujenga barabara za kisasa.

Waziri Dk. Khalid aliwataka wananchi kuwa wastahimilivu katika kipindi hiki ambacho serikali inaendelea na ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kutoa ushirikiano kwa makandarasi wanaojenga miradi hiyo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Habiba Hassan Omar, alisema ujenzi wa Barabara ya Mazizini hadi Maungani ipo katika mradi wa ujenzi wa barabara za ndani.

# ZHC: Tutajenga nyumba za makazi, biashara Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Nyumba Zanzibar (ZHC) limesema litaendelea kujenga nyumba za makazi na biashara katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Shaban Othman, wakati wa uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa nyumba namba 1293/1294 katika eneo la Darajani Mjini Unguja.

Alisema wajibu wa kila mwananchi kushirikiana na kuiunga mkono serikali katika jitihada hizo na kulitaka Shirika la Nyumba kujitahidi kujenga nyumba zenye viwango na ubora.

Aidha, alisema Shirika la Nyumba litaendelea kuzifanyia matengenezo na hata kuzivunja na kuzijenga upya nyumba zote ambazo zimepoteza uhalisia wa kuishi na ambazo ni hatari kwa maisha ya watu.

**Aidha, alisema kutokana na ongezeko la watu kila mwaka serikali imeamua kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya kuwapatia wananchi kwa njia ya kuuza au kukodisha.**

Aidha, alisema kutokana na ongezeko la watu kila mwaka serikali imeamua kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya kuwapatia wananchi kwa njia ya kuuza au kukodisha.

Aliwataka wananchi kuhamasika kununua au kukodi nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba ili kusaidia serikali katika mipango mizuri ya matumizi ya ardhi.

Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba, Sultan Said Suleiman, alisema ujenzi wa nyumba hizo ni hatua ya kuunga mkono jitihada za serikali za kuendelea kuuhifadhi Mji Mkongwe na kuimarisha biashara ya utalii.

Alisema Mji Mkongwe ndiyo sura ya Tanzania bali pia ni sura ya Afrika ya Mashariki, hivyo kuna kila sababu ya kuhakikisha nyumba zilizomo katika mji huo zinakuwa katika hali nzuri.

Alisema Shirika la Nyumba litaendelea na jitihada za kutekeleza maagizo ya serikali kuhakikisha Mji Mkongwe unakuwa mzuri kwa kuhakikisha nyumba zote zinazomilikiwa na shirika hilo zinafanyiwa ukarabati na kujengwa upya.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia , Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Riziki Pembe Juma, (kulia), akiweka jiwe la msingi nyumba za wafanyakazi wa Hospitali ya Wilaya Pangatupu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, mwishoni mwa wiki, ikiwa ni shamrashamra za kuelekea kilele cha miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamu wa Rais asisitiza uwezeshaji wananchi kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu kuendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi, ili kuzitumia fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta ya utalii.

Alisema hayo Msitu wa Masingini Wilaya ya Magharibi A Unguja alipoweka jiwe la msingi la mradi wa utalii rafiki na mazingira unaomilikiwa na Kampuni ya Zanzi Eco- Tourism. Mradi huo una thamani ya Sh.900,000,000.

Alisema Zanzibar kupitia rasilimali za asili kama vile misitu upo uwezekano mkubwa wa wananchi kuwekeza na kupata faida na kwamba kampuni iliyoanza kuwekeza kwenye Msitu wa Masingini imeonesha njia.

Hivyo, alisema suala la hifadhi ya mazingira ni muhimu kwa maisha ya wanadamu na kwamba kampuni hiyo ni vyema ikapanua wigo wake na kuwekeza sehemu nyengine katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Alizitaka Wizara ya Kilimo na mamlaka zinazohusika na uwekezaji kutafuta wawekezaji wengine zaidi kuwekeza katika miradi rafiki na mazingira kwenye misitu tofauti ya hifadhi iliyopo katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Hata hivyo, alisisitiza umuhimu wa mamlaka zinazohusika na hifadhi ya misitu kuendelea kuilinda msitu huo wa Masingini kwa kuwa ni chanzo kikubwa cha upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis alisema mradi huo utasaidia kukabili changamoto ya uharibifu wa mazingira.

Alisema pia mradi huo utaibua fursa zaidi ya kuongeza vivutio vya utalii ili kufikia matumaini ya taifa katika suala la kukuza ajira kwa wananchi.

Mmiliki wa mradi huo, Alan Peter, alisema mbali na hifadhi ya mazingira mradi huo utakuwa na faida kubwa kwa wanawake kusaidia ajira.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi huo, utakuwa na daraja la kuangalia msitu, mgahawa, nyumba ya juu ya miti, daraja la kunesanesa na vivutio vingine.

## HABARI PICHANI



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kijiji cha Nyuki Ltd kilichopo Manispaa ya Singida, Philemon Kiemi, akitoa maelezo juzi kwa Jumuiya ya Wanafunzi waliosoma Shule ya Sekondari Mwenge kuanzia 1991 hadi 1994 walipotembelea katika kijiji hicho kwa ajili ya kujifunza katika sekta ya ufugaji nyuki. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**



Katibu Tawala Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Rashid Mohamed Rashid, akikabidhi jana zawadi za sabuni, mchele, madaftari, kalama, penseli, pasi, mafuta ya kupaka, mikeka na vichongeo kwa viongozi wa kituo cha watoto wenye uhitaji maalum kilichoko Shule ya Msingi Dung'unyi wilayani humo. Mbali na vitu hivyo pia walikabidhiwa mbuzi. Vitu hivyo vimetolewa na wilaya kumuungana mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwakumbuka wenye uhitaji katika kipindi hiki cha sikukuu za Mwaka Mpya. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**



Mwananchi akichagua nguo za sare ya shule za msingi kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao, Manzese jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEONITA JOHNI SANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T526 CPY** aina ya **Toyota WISH,** Chassis No. **ZNE100116402,** Engine No.1ZZ1681445, Capacity..1790 . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MBE/MBE/9125/2024**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ERADIUS BASHARA FULUBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC930ECJ** aina ya **BAJAJ BOXER.** Chassis No. **MD2B15BX4PWE94283,** Engine No. **JVXWPE93767.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/273109/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
27/12/2024

### TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe **30-12-2024** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** Bahari beach kuelekea **DAR ES SALAAM** Mloganzila, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 18.00**
**Upana - mita 2.86**
**Kimo - mita 4.95**

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM Bahari beach** hadi **DAR ES SALAAM Mloganzila** kupitia **Bagamoyo ROAD.**

Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## SIKU TANO KUMALIZA MWAKA 2024;

# MBAYA KWA HISTORIA SAFARI ZA NDEGE

Na Christina Mwakangale

WIKI hii ya mwisho wa mwaka 2024 kwa wakazi wa nchi mbili, Korea Kusini na Azerbaijan ni ya simanzi.

Ajali za ndege katika nchi hizo, imetanguliwa na ile ya Azerbaijan Airlines, ikiwa na abiria 67 huku 38 kati yao wakipoteza maisha, ilitokea mapema asubuhi ya sherehe ya Krismasi.

Ajali ya pili ni iliyotokea jana, ndege ya Shirika la Jeju Air la Korea Kusini, imeongeza majonzi miongoni mwa wakazi wa nchi hizo, huku ajali hiyo ikisababisha vifo takribani 180.

Kwa ajali hizo ni takribani watu 220 waliokuwamo walifariki dunia kwa kipindi cha siku tano.

Usafiri wa anga ni kati ya ulio salama, ukilinganishwa na mwingine kama vile wa ardhi (barabara na reli) pamoja ule wa kwenye maji (meli).

Narscent Meena, ni rubani binafsi katika mazungumzo ya awali na Nipashe, anasema usalama wa usafiri wa anga pia huwa na tahadhari za kuchukua kabla na wakati wa safari za angani.

"Kwanza kila ndege au helikopta kabla haijaruka tunaangalia abiria itabeba watu wangapi, ili ndege iwe na uwiano na inakwenda wapi itaruka futi ngani, mafuta kiasi gani itabeba.

"Pia, mhandisi anaikagua, anajidhihirisha kabla ndege haijaondoka iko sawa, anasaini na kuikabidhi kwa rubani. Kuna watu wa 'road control' wanahakikisha uwiano inaporuka na kutua kama uko sawa," anasema.

Anasema kwamba pamoja na ajali za ndege kufululiza, bado usafiri wa anga ni salama, akisema mabadiliko ya hali ya hewa ghafla pamoja kupoteza mawasiliano, huweza kumwathiri rubani.

"Tatizo la kiafya huweza kumwathiri rubani ghafla na pia rubani kuimani ndege yake inaweza kufanya kazi vizuri, ila tahadhari huchukuliwa bila kujali imebeba viongozi au la."

AJALI KOREA KUSINI

Chanzo cha ajali ya ndege ya Jaju Air, hapo jana bado hakijajulikana. Vyombo vya habari nchini humo vinaripoti kuwa huenda, ilisababishwa na ndege kukamatwa kwenye mfumo wa ndege hiyo.

Kampuni ya kutengeneza ndege ya Boeing, imetoa rambirambi zake na kusema inawasiliana na Jeju Air ya Korea Kusini, baada ya kutokea kwa ajali mbaya ya ndege.

Jeju Air Co., Ltd, ni shirika kubwa la ndege la bei ya chini kwa nchi ya Korea Kusini.

Imepewa jina la Kisiwa cha Jeju. Shirika hilo la ndege lina makao yake makuu katika Jiji la Jeju na kituo chake kikubwa zaidi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jeju.

Pia ni mwanachama mwanzilishi wa Value Alliance.

Ajali hiyo ilihusisha ndege aina ya Boeing 737-800, kwa mujibu wa Jeju Air, si ya kawaida kwa Korea Kusini, ambayo imekuwa na rekodi nzuri ya usalama wa ndege katika miaka ya hivi karibuni.

Ikiwa idadi ya vifo itathibitishwa, itakuwa ni ajali mbaya zaidi ya ndege kuwahi kutokea katika ardhi ya Korea Kusini.

Inaonekana pia kuwa ajali mbaya pekee ambayo Jeju Air imepata katika historia yake ya karibu miaka 20.

Jeju Air, ndilo shirika maarufu la ndege la bei nafuu nchini Korea Kusini, lenye safari nyingi za ndege katika eneo lote la bara la Asia.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, alisema katika mkutano na wanahabari hapo awali shirika hilo la ndege halikuwa na historia ya ajali. Ameomba msamaha kwa familia za waathiriwa.



Timu ya waokoaji wakibeba miili ya abiria katika eneo la ajali, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Muan, Korea Kusini jana. **PICHA: ALJAZEERA**

**AJALI YA NDEGE AZERBAIJAN**

Nchini Azerbaijan, nako kumekuwa ni wiki mbaya kwa wakazi wa nchi hiyo, baada ya ajali ya Desemba 25, mwaka huu, ndege yenye namba J2-8243 iliyopaa kutoka uwanja wa ndege wa Baku, mji mkuu wa Azerbaijan, ikipata ajali.

Ilitarajiwa kutua Grozny, mji mkuu wa mkoa wa Russia wa Chechnya.

Azerbaijan Airlines, pia linajulikana kama AZAL, ndio wabeba bendera na shirika kubwa la ndege la nchi ya Azerbaijan.

Liko Baku, karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Heydar Aliyev, ni mtoa huduma anayefanya kazi katika maeneo mbalimbali ya bara la Asia, Jumuiya ya Madola Huru (CIS) na Ulaya.

Azerbaijan Airlines ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga.

Shirika la ndege hilo, lilianzishwa tarehe Aprili 7, mwaka 1992 kama shirika la kwanza la ndege la kitaifa kuanzishwa, baada ya nchi kupata uhuru wake.

Kampuni hiyo inayomilikiwa na serikali ilibinafsishwa katika miaka ya 2000 na umiliki wa mali za kampuni hiyo, uliishia mikononi mwa kampuni zinazomilikiwa na wanafamilia wa wasomi wa kisiasa wa Azerbaijan, akiwamo binti wa Rais Ilham Aliyev, Arzu Aliyeva.

Ndani ya ndege hiyo kulikuwa na abiria 67 wengi wao wakiwa raia wa Azerbaijan, pamoja na wale kutoka Urusi, Kazakhstan na Kyrgyzstan. Wengi walipoteza maisha.

Ndege hiyo ilikuwa aina ya Embraer 190, inayoendeshwa na Azerbaijan Airlines.

Ndege ilipokaribia Grozny, iliipitia ukungu mzito, abiria walionusurika wanasema.

Wanaelezea jinsi rubani alivyojaribu kutua ndege mara mbili katika hali hiyo.

Ilikuwa ni katika jaribio la tatu, walionusurika wanasema, walihisi mfululizo wa milipuko kugonga ndege.

"Mara ya tatu, kitu kililipuka...baadhi ya ngozi ya ndege ilikuwa imepeperuka," mmoja aliiambia TV ya Kirussia.

Mhudumu wa ndege kwenye ndege hiyo, Zulfuqar Asadov, aliviambia vyombo vya habari vya ndani athari za shambulio hilo "zilisababisha hofu ndani".

"Tulijaribu kuwatuliza [(abiria), ili kuwaondoa wasiwasi. Wakati huo, kulikuwa na shambulio jingine, na mkono wangu ulijeruhiwa," alisema.

Video iliyorekodiwa katika ndege na abiria ilionyesha barakoa za oksijeni zikining'inia kutoka kwenye dari la ndege.

Waziri wa Uchukuzi wa Azerbaijan, Rashad Nabiyev, alisema: "Wote walionusurika walisema walisikia sauti tatu za mlipuko wakati ndege ilipokuwa juu ya anga ya Grozny."

Alisema ndege hiyo iliathiriwa nje na kuharibika ndani na nje ilipokuwa ikijaribu kutua.

Katika wiki za hivi karibuni, Ukraine imekuwa ikilenga Chechnya na maeneo mengine ya Caucasus ya Russia kwa mashambulizi ya drone.

Baada ya ajali hiyo, mamlaka huko Moscow ilisema mashambulizi kama hayo yalisababisha itifaki ya kufunga anga ya juu ya Grozny.

Kulingana na maofisa wa eneo hilo, ndege isiyo na rubani ilidunguliwa na walinzi wa anga juu ya duka kubwa huko Vladikavkaz, karibu na Ossetia Kaskazini, asubuhi hiyo.

Baada ya tukio hilo huko Grozny, ndege ilielekezwa kwa takriban kilomita 450 (maili 280) mashariki hadi uwanja wa ndege wa Aktau huko Kazakhstan. Bado haijulikani kwa nini ilielekezwa kwenye Bahari ya Caspian, safari ndefu zaidi kuliko chaguzi zingine kadhaa.

Mamlaka ya anga ya Russia, imedai marubani wa ndege hiyo walipewa viwanja vingine vya ndege, lakini wakachagua Aktau.

Data iliyotolewa na tovuti ya ufuatiliaji wa safari za ndege ya Flight Radar, inaonyesha ndege hiyo ikiyumbayumba juu na chini ilipokaribia Aktau, kabla ya kugeuka na kutua kilomita chache kutoka uwanja wa ndege.

Video kutoka karibu na eneo la tukio inaonesha ndege hiyo, ikishuka kwa kasi angani kabla ya kuanguka ardhini na kusereka kwa mita 100 kadhaa ikiwa inawaka moto.

Watu 38 waliuawa na 29 walinusurika, wengine wakiwa na majeraha mabaya. Ajabu ni kwamba baadhi ya walionusurika walionekana wakitembea na kutambaa kutoka kwenye mabaki ya ndege hiyo.

Marubani wa ndege hiyo wanasifiwa kwa kuokoa maisha kwa kufanikiwa kutua sehemu ya ndege hiyo, licha ya wao kuuawa kwenye ajali hiyo. Inaaminika wengi walionusurika walikuwa wameketi nyuma yake. Ripoti za awali zilidokeza kuwa ndege hiyo iligongana na kundi la ndege.

Hata hivyo, wataalamu wa masuala ya usafiri wa anga na watu wengine nchini Azerbaijan wanaamini kuwa mifumo ya GPS ya ndege hiyo, iliathiriwa na msongamano wa kielektroniki na kisha kuharibiwa na vipande vya milipuko ya makombora ya ulinzi wa anga ya Russia.

***Uchambuzi, kwa msaada wa vyombo vya habari kimataifa***

# Djuma aanika ya Namungo

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa kulia wa Namungo FC, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Djuma Shaaban, ameeleza kuwa kuachwa kwake na klabu hiyo kunatokana na majeraha ya mara kwa mara yanayomsumbua.

Alisema ni yeye mwenyewe ndiye aliyeomba asitishiwe mkataba wake wa miezi sita uliobaki ili apate muda mzuri na kujiuguza na kuwa fiti.

Alisema majeraha ambayo yamekuwa yakimwandama na kumfanya awe zaidi kwenye chumba cha matibabu kuliko uwanjani.

**"Nimekaa nje kwa muda mrefu, sikupata muda mrefu wa kuitumikia Namungo kutokana na kuwa majeruhi, nime amua kuomba waniache ili nipate muda mrefu wa kujitibia nipone ka bisa na kuanza kuj weka fiti bila kuwa na presha yoyote, natumaini baada ya hapo nitaru di nikiwa fiti zaidi," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Yanga. Beki huyo alijiunga na Namungo mwanzoni mwa msimu huu kwa mkataba wa mwaka mmoja akiwa mchezaji huru.**

Kabla ya hapo aliichezea Yanga kuanzia 2021 hadi 2023, akitokea Klabu ya AS Vita za DRC, ambayo alijiunga nayo 2017 akitokea FC Renaissance pia ya huko.

Wakati Djuma akiondoka kwenye timu hiyo kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, klabu hiyo inaendelea na usajili ikiwa tayari imesajili wachezaji kadhaa ambao baadhi wameanza kuonekana uwanjani.

Wachezaji hao ni Najib Mussa kutoka Singida Black Stars, Derrick Mukombozi, Emmanuel Charles, ambao wamerudishwa tena kwenye kikosi hiyo baada ya kuwamo msimu uliopita na kuachwa mwanzoni mwa msimu huu, pamoja na beki wa kati na kiungo mkabaji wa zamani wa Azam FC, Daniel Amoah.

# MABADILIKO YA KATIBA TOC YAPITA, UCHAGUZI MWAKANI

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JUMLA ya wanachama 39 wa vyama na mashirikisho ya michezo hapa nchini yaliyo chini ya Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), wameridhia na kupitisha mabadiliko ya katiba, katika Mkutano Mkuu wa kawaida uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma.

Kutokana na mabadiliko hayo, TOC inatarajia kufanya uchaguzi mkuu mapema mwakani kwa kutumia katiba hiyo iliyopitisha baada ya kuidhinishwa na serikali.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo jijini hapa, Rais wa TOC, Gulam Rashid, alisema vyama na mashirikisho ya michezo vinapaswa kuwa wanachama hai katika mashirikisho ya michezo ya kimataifa ili watambulike ikiwamo kushiriki mashindano ya kimataifa ya mchezo husika.

Aidha, alisema wakifanya hivyo kwa kufuata kalenda za vyama vyao pamoja na zile za kimataifa kutasaidia kuwa na timu nzuri za taifa ambazo zitaitangaza nchi katika maeneo mbalimbali duniani.

"Vyama na mashirikisho mnapaswa kuzingatia hili, mkitoka hapa mkafanye mabadiliko ili kupiga hatua katika mchezo husika wa chama au shirikisho," alisema Rashid.

Naye Katibu Mkuu wa TOC, Filbert Bayi, alisema TOC kwa kushirikiana na 'Olimpiki Solidariti' (Olympic Solidarity), hadi kufikia mwisho wa kufikia viwango, bado iliendelea kudhamini wanamichezo waliofikia viwango vya kushiriki michezo ya Olimpiki ya Paris 2024.

Alisema wanafanya hivyo ili kuhakikisha michezo inazidi kupiga hatua hapa nchini hususan katika uwakilishi wa wachezaji kimataifa.

Bayi alisema mapema 2022 Olimpiki Solidariti kupitia Kamati ya Olimpiki Tanzania ilitoa udhamini wa maandalizi ya Paris 2024 kwa wanamichezo watano wa mchezo wa riadha, (Alphonce Simbu, Gabriel Geay na Failuna Matanga, na kwa upande wa Judo ni Andrew Thomas Mlugu huku kuogelea akiwa ni Hilal Hemed Hilal.

Alifafanua zaidi ya kuwa wanariadha wawili wa kike Magdalena Shauri na Jackiline Sakilu, baada ya kufikia viwango walifaidika na udhamini wa miezi saba kuanzia Januari-Julai, 2024 kuboresha muda wao ili waweze kufanya vizuri katika michezo ya Paris 2024.

Bayi alisema pamoja na kuusimamisha uongozi wa Ngumi za Ridhaa (BFT), kutokana na matumizi mabaya ya fedha walizopewa kwa ajili ya matumizi ya wachezaji kushiriki mashindano ya dunia yaliyofanyika Tashkent, Uzbekistan, mwaka 2023, Kamati ya Olimpiki Tanzania imeendelea kutoa udhamini kwa mchezaji Yusufu Lucasi Changalawe kwa kumpeleka kwenye mashindano ya kutafuta viwango (qualifying competition) vya kushiriki Paris 2024 yaliyoandaliwa na IOC katika nchi za Italia na Thailand, lakini hakuweza kufanikiwa kufikia viwango hivyo.

ZUCHU...




Daktari Bingwa wa magonjwa ya moyo, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Peter Kisenge, akimfanyia vipimo mbalimbali vya moyo msanii wa Muziki, Zuchu, wakati alipotembelea taasisi hiyo mwishoni mwa wiki kupata huduma hiyo ya vipimo bure fursa ambayo imetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan. **MPIGAPICHA WETU**

# Wasanii wamiminika JKCI ofa ya Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

WASANII wameendelea kuchangamkia fursa ya kupima moyo bure katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), iliyotolewa na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza wakati wa uchunguzi wa moyo kwa wasanii hao jana, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Peter Kisenge, alisema amefurahi kuona wasanii wanachangamkia fursa hiyo na kuwataka wengine kuendelea kujitokeza.

"Nimemwona Zuchu, Mboso, D Voice, wamekuja naomba nitumie fursa hii kuwashauri wasanii wengine waige mfano huu wa kuja kupima vipimo vya moyo bure," alisema.

"Tunamshukuru sana Rais Samia kwa fursa hii ya kuwapima wasaniii bure, hii ni kuhamasisha wananchi wote wawe na tabia ya kupima afya zao ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanachangia vifo vingi sana," alisema.

Naye Mbwana Yusufu kutoka (WCB), maarufu Mboso, alisema yeye anashida ya moyo na amekuwa akifanya vipimo mara kwa mara kujua maendeleo ya afya yake.

"Binafsi najifahamu nina matatizo ya moyo na ninaendelea na matibabu madogo madogo, nimefanya vipimo na nimeonekana bado ninashida, nitafanyiwa vipimo zaidi na wameahidi kutatua changamoto yangu," alisema.

"Namshukuru sana Rais Samia kwa kutupa fursa hii nawaomba wasanii waje kujua kama wanachangamoto ya moyo wasiogope kwasababu hapa ni vipimo na ukigundulika unashida unapatiwa matibabu," alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa nchini (BASATA), Dk. Kedmon Mapana, aliwashukuru wasanii kwa kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa hiyo iliyotolewa na Rais Samia na alimshukuru pia Dk. Kisenge kwa kufanikisha upimaji huo.

"Tunamshukuru na kumpongeza sana Dk. Kisenge kwa kuratibu zoezi hili maana wasanii wamekuwa wakija hapa JKCI na nimeona Diamond akihamasisha wasanii wengi waje na leo ameleta pia kundi la wasanii wa lebo yake," alisema.

HABARIMICHEZO

## ZISIKUPITE

### VAN DE VEN NA MADRID

BEKI wa Tottenham Hotspur na Uholanzi, Micky van de Ven mwenye umri wa miaka 23, analengwa na Real Madrid katika dirisha la Januari baada ya kuwa na majeruhi wengi wa safu ya ulinzi wa klabu hiyo. ***(Relevo)***

### RAMOS ATAKA KUREJEA

NAHODHA wa zamani wa Real Madrid, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 38 ana nia ya kurejea tena kwa miamba hao wa Santiago Barnabeu kutokana na timu hiyo kukumbwa na majeruhi wengi, Dani Carvajal miaka 32, David Alaba (32) na Eder Militao (26). ***(AS)***

### OLMO KWENDA EPL

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 26, yuko tayari kuhamia kwa mkopo kwenye Ligi Kuu England Januari kama klabu yake haitaweza kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania kwa kipindi cha pili cha msimu. ***(TBR Football)***

### STERLING HAONDOKI

MSHAMBULIAJI wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 30, hatafikiria kukatiza mkataba wake wa mkopo na Arsenal kutoka Chelsea Januari, licha ya kutoanza mchezo wa ligi tangu Oktoba 19. ***(Athletic)***

### VINICIUS JR MKATABA MPYA

REAL Madrid inapanga kufanya mazungumzo na mshambuliaji wa Brazil, Vinicius Jr mwenye umri wa miaka 24 kuhusu mkataba mpya. ***(AS)***

### DE BRUYNE KUHAMIA MAREKANI

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 33, anapendelea kuhamia Marekani, mara mkataba wake utakapomalizika msimu huu. ***(Teamtalk)***

### BALOTELLI ATAKIWA MEXICO

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester City, Mario Balotelli mwenye umri wa miaka 34, anasakwa na Klabu ya Mexico, Cruz Azul - ambayo itakuwa klabu ya 13 katika maisha ya Muitaliano huyo. ***(Gazzeta dello Sport)***

### BRANTHWAITE BADO ALENGWA

KLABU ya Everton bado haijaanza mazungumzo ya mkataba na beki wa England, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 22, ambaye analengwa na Liverpool, Manchester United na Manchester City. ***(Daily Mail)***


### ROBINSON AWANIWA

LIVERPOOL inafuatilia hali ya beki wa kushoto wa Fulham, Antonee Robinson, na uwezekano wa kumnunua beki huyo wa Marekani mwenye umri wa miaka 27 Januari. ***(Football Insider)***

### DURAN KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 21, anaweza kuondoka Aston Villa katika dirisha la uhamisho, huku mshambuliaji wa Atalanta mwenye umri wa miaka 25 raia wa Italia, Mateo Retegui akichukuliwa kama mbadala wake. ***(Caught Offside)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KOCHA GUARDIOLA: SITAKATA TAMAA

●●●Bila shaka nataka kushinda tu, kila mtu anataka hivyo, sitaki kuwakatisha tamaa watu wangu kwa...

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesisitiza kuwa “sitakata tamaa“ katika harakati zake za kiurudisha Manchester City katika njia ya ushindi baada ya klabu hiyo kushinda mechi moja tu katika 13 zilizopita kwenye michuano yote.

Sare ya nyumbani ya City ya bao 1-1 dhidi ya Everton siku ya Boxing Day iliwaacha chini katika nafasi ya saba, pointi tano kutoka kwenye nafasi nne za juu na 14 nyuma ya viongozi Liverpool, ambao wana mchezo mkononi.

Guardiola alisema wiki hii kuwa City wako katika hatari ya kukosa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu katika hali ambayo itakuwa ya kushangaza kwa mabingwa hao watetezi.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 53, ambaye alitia saini nyongeza ya mkataba ya miaka miwili mwezi uliopita, alisema licha ya matokeo duni, lakini hakujaathiri nia yake ya kuirejesha City kwenye kiwango chake cha awali.

“Sitakata tamaa. Nataka kufanya hivyo. Na kwa hali tulizo nazo, lazima tufanye hivyo,“ alisema Guardiola.

“Bila shaka nataka kushinda tu. Kila mtu anataka hivyo. Sitaki kuwakatisha tamaa watu wangu, kwa upande wa klabu, mashabiki, au watu wanaoipenda klabu hii.“

Guardiola alisema matokeo ya kushtua ya timu yake, kipindi kibaya zaidi katika maisha yake ya ukocha yamemsaidia kutambua jinsi walivyokuwa wazuri katika harakati zao za kushinda mataji manne mfululizo ya Ligi Kuu England.

“Hiyo inanifanya nikumbuke jinsi zamani ilivyokuwa nzuri,“ alisema.


„Huo ndio ukweli, ambao umenifanya nitambue sasa tumefanya nini, kwa sababu wakati mwingine una majeraha.

“Lakini unatarajia nini. Hatukutarajia hali hii na sababu kuu ni kuwa na wachezaji saba au nane muhimu ni majeruhi.

“Lakini naona ari ya timu katika mazoezi, jinsi walivyo makini, naamini tutarudi kwenye ubora wetu.“

## Alexander-Arnold sasa aweka wazi kuondoka Liverpool

**LIVERPOOL, England**



TRENT Alexander-Arnold ameripotiwa kuwaarifu Liverpool kuhusu nia yake ya kujiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa ripoti.

Beki huyo wa kulia amebakiwa na siku kadhaa kabla ya kuingia katika miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na Madrid wanaweza kumpata bure mwishoni mwa msimu huu.

Iliripotiwa mapema mwezi huu kwamba Alexander-Arnold, licha ya kupewa mkataba mpya na Liverpool, "anashawishiwa" na wazo la kuhamia Santiago Bernabeu mwishoni mwa msimu.

Gazeti la Marca limeripoti kuwa tayari Arnold amewataarifa Liverpool kwamba anataka kujiunga na Madrid, akiwafahamisha waajiri wake wa sasa kuhusu uamuzi wake huo wakati wa jaribio lao la kumshawishi kuongeza mkataba.

Liverpool walitaka kuingia 2025 wakiwa na uhakika kamili kama Alexander-Arnold atasaini mkataba mpya, na inaonekana kama beki mpya wa kulia atakuwa kwenye orodha yao ya usajili wa wachezaji katika miezi ijayo.

Macho yote sasa yataelekezwa kwa Liverpool wanapoamua kukaribisha ofa kwa Alexander-Arnold mnamo Januari.

Madrid, kwa upande wao, hawataanzisha uhamisho wa majira ya baridi na badala yake watasubiri kuona kama Alexander-Arnold akitua kwao kwa usajili wa bure.

## De Jong haondoki Barca – Wakala

**BARCELONA, Hispania**

WAKALA wa kiungo wa kati wa Barcelona, Frenkie de Jong, amekanusha uvumi wa uwezekano wa mteja wake kuondoka katika klabu hiyo.

Mustakabali wa De Jong umekuwa suala la uvumi usiokoma kwa miaka ya hivi karibuni sasa anapoingia miezi 18 ya mwisho ya mkataba wake, huku hali ya sintofahamu ikiongezeka zaidi.

Nafasi yake ndogo ya kucheza chini ya kocha mpya, Hansi Flick, imekoleza mafuta kweye moto kuhusu uvumi wa kuondoka.

Hivi karibuni gazeti la AS liliripoti kwamba wakala wa De Jong, Ali Dursun, alikuwa akichunguza uwezekano wa uhamisho wa kwenda Saudi Arabia, huku Mholanzi huyo akidai kuwa anavutiwa na utajiri wa ofa katika Ligi ya Saudi Pro League.

Hata hivyo, Dursun mwenyewe sasa amepuuzilia mbali uvumi huo, akiiambia De Telegraaf: "Mazungumzo nchini Saudi Arabia? Upuuzi mtupu. Inaondoa tamaa ya kweli ya Frenkie.

"Anataka jambo moja tu: kuwa fiti ili kung'ara kwa muda mrefu katika klabu anayoipenda ya Barcelona na anahisi yuko nyumbani."

Licha ya De Jong kutaka kubaki Barcelona, kumekuwa na ripoti nyingi zinazosema 'Blaugrana' hao wanataka kumtoa De Jong ili kupunguza matumizi kwa sababu ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa mshahara mkubwa zadi.

# MAN UNITED WASAKA MBADALA WA ONANA




**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeanza kuwasaka makipa wapya, ripoti imefichua, huku Andre Onana na Altay Bayindir wanapigania mustakabali wao hapo Old Trafford.

Onana amekuwa chaguo la kwanza pale Man United tangu kujiunga na timu hiyo kwa pauni milioni 47.2 kutoka Ajax katika msimu wa majira ya joto wa 2023.

Muda wake wa uchezaji umekumbwa na makosa mengi binafsi, hasa tangu kuwasili kwa Kocha Mkuu mpya, Ruben Amorim.

Kipa namba mbili nyuma ya raia huyo wa Cameroon, Bayindir, ameshindwa kutamba katika nafasi yake.

Nafasi imekuwa ndogo, lakini Onana anaonekana kuwa na makosa mengi zaidi.

Kwa mujibu wa gazeti la Telegraph limefichua Man United imeanza kutathmini chaguo lao jipya, huku mlinda mlango wa Royal Antwerp, Senne Lammens mwenye umri wa miaka 22, akiwekwa kwenye rada.

Lammens amekuwa kwenye kiwango bora, huku Borussia Dortmund ikisemekana pia kuitaka saini yake.

Ingawa kwa sasa Man United haitaingia haraka kusajili golikipa mpya – kwani kipaumbele kikubwa ni beki wa kushoto, huku Nuno Mendes wa Paris Saint-Germain akilengwa.

HABARI MICHEZO

# TANZANIA YAMALIZA 2024, KWA REKODI, TIMU 7 ZAFUZU KIMATAIFA

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2024 umeonekana kuwa ni wa mafanikio makubwa kwenye soka la Tanzania, ambapo timu zake mbalimbali za taifa zimefuzu kucheza michuano ya kimataifa kitu ambacho ni nadra sana kutokea huko nyuma kwenye mchezo wa mpira wa miguu.

Chini ya uongozi wa rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, timu saba za taifa zimefuzu fainali zake ambazo zingine zimeshachezwa na zingine zitachezwa mwakani.

Wiki iliyopita, Timu ya Taifa Ya soka ya Vijana chini ya miaka 17, Serengeti Boys, ilifuzu kucheza fainali za AFCON chini ya miaka hiyo zitakazofanyika nchini Morocco mwakani.

Hii ni baada ya kuichapa, Sudan Kusini mabao 4-0, katika mchezo wa kusaka kucheza fainali hizo kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki (CECAFA).

Tanzania pia mwaka huu ilifuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Walemavu (BAFCON), yaliyofanyika mwaka huu nchini Misri, hata hivyo michuano hiyo haipo chini ya TFF, lakini moja ya mafanikio makubwa kwa taifa linaloongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kikosi cha Timu ya Taifa chini ya miaka 15, nacho kilifanikiwa kufuzu fainali za shule barani Afrika, huku Tanzania ikiwa mwenyeji.

Timu ya Taifa chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes nayo haikuwa nyuma, kwani imefuzu fainali za AFCON, ambazo zinatarajiwa kuchezwa nchini Ivory Coast.

Kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars, nacho kimefuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (WAFCON), zinazotarajiwa kuchezwa nchini Morocco.

Kama vile haitoshi Tanzania imepeleka fainali timu mbili za soka wanaume, moja ya Wachezaji wa Ndani ya nchi na nyingine ni ya jumla, CHAN.

Kwa upande wa CHAN, Stars ilifuzu fainali hizo zinazotarajiwa kupigwa mwakani katika nchi tatu za Tanzania, Kenya na Uganda kama mwenyeji.

Taifa Stars, timu kubwa ya soka Tanzania yenye wachezaji wote wa ndani na nje, yenyewe ilifanikiwa kufuzu (AFCON), zinazotarajiwa kuchezwa mwakani nchini Morocco.

Rais Samia amekuwa msaada mkubwa katika mafanikio hayo kwa kuzisapoti na kuzipongeza kwa fedha kila zinaposhinda.

# Maxime aishangaa Mashujaa FC

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Dodoma Jiji, Mecky Maxime, ameishangaa Mashujaa FC kushindwa kupata ushindi dhidi yao, katika mchezo wa juzi uliofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma kutokana na makosa mengi ambayo wameyafanya na kushindwa kuyatumia.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika kwa Dodoma Jiji kuichakaza Mashujaa FC mabao 3-1, Maxime, alisema makosa ambayo safu yake ya ulinzi ilikuwa inayafanya, kama ingekutana na timu kubwa kama Simba, Yanga, Azam na hata Singida United, hali ingekuwa nyingine.

"Niwapongeze wachezaji wangu, lakini bado nipo pale pale, tumeendelea kufanya makosa yale yale, tumeshinda mabao matatu, lakini tumefanya makosa mengi, kipindi cha kwanza tumefanya manne, ukikutana na timu kama Simba, Yanga, Azam na Singida Black Stars wanakuadhibu, unafunga mabao matatu wao wanakufunga manne.

"Nadhani ni wao wenyewe tu Mashujaa wameshindwa kutuadhibu, nashangaa wameshindwa kutumia zile nafasi, na moja walibaki watatu na kipa, ilikuwa ni kuuweka wavuni, wakaukosa, kwa maana hiyo bado tuna kazi kubwa ya kufanya, lazima tupunguze makosa," alisema Maxime.

Yalikuwa ni mabao ya Mwana Kibuta, dakika ya 12, Lulihoshi Heritier dakika ya 16, na Zidane Sereri dakika ya 83, bao la kufutia machozi la Mashujaa FC likiwekwa ndani ya wavu na Crispin Ngushi dakika za majeruhi.

Matokeo hayo yameifanya timu hiyo kufikisha pointi 19, ikiwa nafasi ya tisa ya msimamo, ikiiacha Mashujaa ikiwa nafasi ya saba na pointi hizo hizo 19.

Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohamed Abdallah ,Bares', alilalamika kutokuwa na utulivu kwenye safu yake ya ulinzi kitu ambacho kimesababisha kupoteza mechi hiyo.

"Mabao mawili ya haraka haraka yalitutoa mchezoni, ndiyo yaliyotuhukumu kupoteza mechi hii, hatukuwa watulivu tangu mwanzo na hatukuwa makini sehemu ya ulinzi," alisema kocha huyo.

## IKAWE YA BARAKA...



Beki wa kushoto wa Simba, Valentin Nouma, wakipozi katika picha na mkewe baada ya kufunga pingu za maisha wiki iliyopita nchini kwao Burkina Faso. **PICHA: MTANDAO**

# Fadlu awaahidi Simba makubwa

INATOKA UK. 24

hadi kesho watakapoanza tena mazoezi kwa ajili ya mechi ya Kombe la Shirikisho dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia ugenini.

"Ulikuwa ni mchezo mzuri, nimefurahia kiwango cha wachezaji wangu, hatuwezi kulalamikia uwanja kwa sababu tunatakiwa kucheza kutokana na mzingira tunayoyakuta, tumeumaliza na sasa tunaangalia michuano ya CAF.

„Nimewapa mapumziko wachezaji wangu hadi Jumanne tutakapoanza tena kujiandaa na mechi dhidi ya CS Sfaxien," alisema Fadlu.

Kaimu Kocha Mkuu wa Singida Black Stars, Ramadhani Nsanzurwimo, alisema kila timu ilicheza vema kipindi kimoja, wapinzani wao wakitawala kipindi cha kwanza na wao cha pili, pia kushindwa kuwazuia Simba kwenye mipira ya faulo na kona kama walivyofanyia mazoezini.

"Kipindi cha kwanza Simba walicheza vizuri kwa sababu tulipoteza sana mipira, cha pili tulijitahidi kucheza, lakini uwanja haukuwa mzuri.

"Siku hizi Simba wanafunga mabao yao kwa njia ya kona na faulo, tulifanyia sana mazoezi jambo hilo, lakini kwa bahati mbaya na sisi tumeadhibiwa," alisema.

Wakati Simba ikiwa kileleni kwa pointi 40, Singida Black Stars ipo kwenye nafasi ya nne ikisalia na pointi 33.

# Yanga yafunga mwaka kwa 5G

INATOKA UK. 24

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko ya wachezaji kwa nyakati tofauti, lakini haikuisaidia Fountain Gate ambayo ilikuwa ikicheza nyuma ya mpira hata ilipokuwa imefungwa idadi hiyo ya mabao.

Shiga, alijifunga dakika ya 53 na kuipa Yanga bao la nne, akiusindikiza kwa kifua mpira uliokuwa unarudi uwanjani baada ya shuti la Pacome kugonga mwamba wa juu na kuwa bao la tano, wachezaji wakijifunga wenyewe kwenye Ligi Kuu.

Dakika tatu kabla ya mechi kumalizika, Mzize alipachika bao la tano kwenye mchezo huo, likiwa la sita kwake msimu huu akiwa sasa anaongoza kwa ufungaji mabao kwenye kikosi cha Yanga.

Aliwazidi mbio mabeki wa Fountain Gate na kuubetua mpira mbele ya kipa Noble aliyekuwa ametoka langoni kumkabili, mpira ukaelekea wavuni licha ya jitihada za Laurian Makame kutaka kuuokoa.

Kipigo hicho kinaiacha Fountain Gate ikiwa na pointi 20, ikiwa kwenye nafasi ya sita ya msimamo wa ligi ambayo imeanza kuingia mzunguko wa pili kwa baadhi ya mechi, huku Yanga ikimaliza mzunguko wa kwanza kwa kukusanya pointi 39.

Baada ya kipigo hicho, taarifa kwa umma iliyotolewa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Fountain Gate, ilieleza kuwa umeamua kulivunja benchi lote la ufundi lililokuwa likiongozwa na Kocha Mkuu, Mohamed Muya.

Michezo
Jumatatu Desemba 30, 2024
Nipashe

## Guardiola: Sitakata tamaa

UKURASA 21





Kiungo mshambuliaji wa Yanga Stephane Aziz Ki, akipasua katika ya msitu wa mabeki wa Fountain Gate, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex. Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda mabao 5-0. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAFUNGA MWAKA KWA 5G

Yavunja benchi lote la ufundi Fountain Gate, huku Mzize akiibuka kinara wao wa mabao kwa kufikisha...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, wamepata ushindi mkubwa zaidi kwa mara ya kwanza, wakiibamiza Fountain Gate mabao 5-0 katika mechi ya upande mmoja muda mwingi wa mchezo iliyochezwa, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

Ni mechi ya tano mfululizo kwa Yanga kupata ushindi tangu ilipofungwa kwa mara ya mwisho na Tabora United mabao 3-1, Novemba 7, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Ushindi huo pia umeifanya Yanga kuwa timu inayoongoza kwa kufunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu, kwani imefikisha jumla ya mabao 32, ikiiacha Simba ikiwa na mabao 31 ya kufunga, lakini kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa zikiwa zimelingana.

Yanga imeruhusu jumla ya mabao sita wakati Simba ikiruhusu matano nyavuni kwake zote zikicheza mechi 15 kila moja.

Hata hivyo, pamoja na ushindi huo, Yanga inaendelea kuwa nafasi ya pili baada ya kufikisha pointi 39, nyuma ya Simba iliyo kileleni na alama zake 40.

Yalikuwa ni mabao mawili ya Pacome Zouzoua, Mudathir Yahaya, Clement Mzize na moja la kujifunga na Jackson Shiga, yalitosha kuwafanya mashabiki wa Yanga kutoka uwanjani maeneo ya Mwenge kwa furaha.

Mechi ilianza taratibu kama vile timu zote zilikuwa zinasomana na hakukuwa na shambulizo lolote hadi dakika ya 14, Pacome alipokosa bao akiwa ndani ya eneo la hatari kwa shuti lake la mguu wa kushoto kutoka nje akiwa amepata pasi mpenyezo kutoka kwa Mudathir.

Dakika moja baadaye kiungo mshambuliaji huyo raia wa Ivory Coast, alisawazisha makosa yake alipofunga bao la kwanza, akiunganisha krosi kutoka wingi ya kushoto iliyopigwa na Shadrack Boka.

Salum Kihimbwa aliikosesha Fountain Gate bao dakika ya 18, alipowalamba chenga, Kibwana Shomari na Dickson Job, lakini alipiga shuti dhaifu lililodakwa na kipa Aboutwalib Mshery.

Faulo iliyopigwa na Stephane Aziz Ki, dakika ya 27, nusura itinge nyavuni, lakini mpira ukagonga nguzo ya pembeni na kutoka nje, huku ukiwa ameshampita kipa, John Noble.

Mnigeria huyo, alifanya kazi ya ziada dakika ya 31, alipofanikiwa kudaka shuti la ana kwa ana la Pacome, alipolipiga akiunganisha mpira wa kona uliopigwa na Aziz Ki.

Kama angekuwa makini, straika Edgar William, angeweza kuipatia Fountain Gate bao dakika ya 34, baada ya kutengenezewa nafasi nzuri na Kihimbwa, akiwa anamtazama kipa Mshery, alichelewa kupiga, na wakati alipoamua kufanya hivyo, beki Ibrahim Hamad 'Bacca' alikuwa amefika na mpira ukambabua na kuwa kona.

Dakika ya 40, Yanga iliandika bao la pili likiwekwa wavuni na Mudathir, likiwa bao lake la kwanza msimu huu. Bao hilo lilipatikana baada ya kutokea kizaazaa kwenye lango la Fountain Gate, kabla ya Prince Dube hajaurudisha ndani mpira uliokuwa unataka kutoka, mfungaji akaukwamisha wavuni.

Pacome, aliiandikia Yanga bao la tatu, likiwa ni la tano kwake msimu huu akipokea pasi kutoka kwa Aziz Ki, ambaye aliukimbilia mpira ulioachwa kizembe na wachezaji wa Fountain Gate.

INAENDELEA UK. 23

## Fadlu awaahidi Simba makubwa

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewaambia wanachama na mashabiki wa Simba watarajie makubwa zaidi mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kumaliza raundi ya kwanza kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 40.

Akizungumza juzi baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu kati ya timu hiyo na Singida Black Stars na kuiongoza kushinda bao 1-0, kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida, lililowekwa wavuni kwa kichwa na Fabrice Ngoma, akiunganishwa mpira wa kona kutoka kwa Jean Ahoua, kocha huyo alisema anakwenda kukiboresha kikosi kwa mara nyingine ili kirejee kikiwa bora zaidi ya kilivyokuwa sasa, hivyo mashabiki watafurahi zaidi.

Huku akiwaomba kuendelea kujitokeza kwa wingi viwanjani kila inapocheza, alisema: „Tumemaliza michezo 15, tumevuna pointi 40, napenda kuwashukuru sana mashabiki wa Simba, kila tunapokwenda, kila tunaposafiri tunao na wengine tunawakuta huko.

"Tunataka kufanya kitu kingine kizuri zaidi mzunguko wa pili, tunaiboresha timu na kuendelea kukinoa kikosi kiwe bora zaidi ya mzunguko wa kwanza, hivyo tunawaomba wanachama na mashabiki wote wa Simba kuwa karibu nasi kwa ajili ya kutupa sapoti."

Fadlu aliendelea kulia na baadhi ya waamuzi kushindwa kulinda wachezaji wake kwa rafu mbaya wanazochezewa, hasa Kibu Denis, ambaye alisema huwa ni mhanga wa kuchezewa rafu za makusudi na wapinzani, lakini waamuzi wamekuwa hawamtendei haki.

"Katika mchezo huu tumenyimwa penalti mbili, Kibu amekuwa muungwana sana, amekuwa akipigwa mabuti, akipigwa viatu na mabeki mbalimbali katika michezo mingi, halindwi, leo hii imekuwa hivyo hivyo, lakini amekuwa akinyanyuka na kuendelea kucheza mpira, waamuzi wanaangalia tu," alilalamika kocha huyo raia wa Afrika Kusini.

Alimlalamikia pia kipa Metacha Mnata kuwa alikuwa anapoteza muda bila sababu yoyote na kupozesha mchezo.

"Kipa wao naye alikuwa anapoteza muda, anapoozesha mchezo kwa kujifanya kaumia, nilikuwa simwelewi, alikuwa anataka timu yake ipate ushindi, pointi tatu, moja au ipate bonasi, sikuwa na uhakika na hilo," alisema. Alisema amefurahishwa na kiwango cha wachezaji wake na amewapa mapumziko baada ya mechi hiyo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042